# HISTORIA FUPI
## FAMILIA YA MT. YOHANE BOSKO

**Kuzaliwa Yohane Bosko**

Mtakatifu Yohane Bosko alizaliwa 16 th Agosti 1815 huko Italia, karibu na mji wa *Castelnuovo*. Anafahamika kwa jina la kipadre Don Bosko maana yake Padre Bosko. Padre Bosko alifariki dunia mnamo 31st Januri 1888. Ni katika siku hiyo aliyokufa tunaadhimisha sikukuu yake. Alizaliwa katika familia maskini. Wazazi wake waliitwa Fransisko Bosko na Margaret Occhiena. Yohane Bosko alikuwa na umri wa miaka miwili wakati Baba yake alipo aga dunia.

Bada ya Fransisko kufa, mama Margaret ndiye alichukuwa majukumu yote ya familia. Kwa kweli mama huyo alikuwa mtu mwema katika roho. Alimwamini Mungu zaidi sana hata katika mahangaiko na shida za kifamilia. Ni mama ambaye aliwafundisha watoto wake imani. Msingi wa imani kwa Mungu, ndio uliwawezesha kupata mahitaji ya familia.

**Margareti Occhiena na Fransisko Bosko**

Margareti Occhiena Alizaliwa 1 Aprili, 7788 huko *Capriglio*. Kwake dini ya karne nyingi, na ibada zake ilikuwa sehemu ya maisha yake. Alikuwa na imani dhabiti katika sakramenti za Kanisa na pia alielewa mambo makuu ya mwisho ambayo yanaunda maisha. Alichukuliwa kwa umuhimu sana mafundisho ya Katekismu yaliyoendelezwa kufundishwa katika mahubiri na kudhihirishwa katika maisha ya kila siku na neema na ya Mungu. Mambo hayo yalikuwa: *Mbingu, kifo, toharani* na *moto wa milele*. Familia yake ilikuwa ya wakulima wa zabibu. Familia yao yote ilifanya kazi kwa bidii. Walikuwa makini sana nyakati za sala hasa ile sala ya saa sita ya Malaika. Familia yao ilikuwa na msingi dhabiti wa imani na sala. Familia ya Margareti Occhiena, kila siku walihudhuria misa bila kuchelewa.

Katika shuguli zao za kila siku waliweze kukutana na familia ya Bosko. Fransisko alizaliwa 4 Februari 1784, katika ya watoto 12 sita walikuwa wamekufa wakati alifikia umri wa miaka sita. Wakati Baba yake alikuwa na umri wa miaka 18. Ilimbidi

achukue majukumu ya kuitunza familia yake. Mwaka 1801, alimuoa Margaret Cagliero ambaye alimzalia watoto wawili, Anthony aliyezaliwa 1 Machi, 1808 na Theresa aliyezaliwa 16 Februari 1810 na akafa siku mbili baada ya kuzaliwa.

Ukoo wa Bosko tangu mwaka 1624, ulikuwa maarufu sana. Walikuwa walinzi wa mfalme na pia kazi ambazo zilihitaji ujuzi wa hali ya juu. Ukoo huu ulijua sana matatizo na mahangaiko ya nyakati zile hasa wakati wa vita. Mama Margareti alikuwa mwanamke mwenye sifa ya sala na bidii katika kuitunza familia yake na hasa aliwachukua watoto wa Fransiko kama wake. Mtu hangefahamu tofauti yoyote kati ya watoto wa Margaret Occhiena na wale wa yule mwanamke marehemu aliyekuwa mke wa kwanza wa Fransisko. Aliwapenda wote na kuwatunza kwa moyo. Aliilea familia yake katika imani. Kila asubuhi walisali, walienda misa na pia aliwaanda vema kwa Sakramenti zote. Alikuwa makini sana kuwaandaa kwa Sakramenti ya kitubio. Alifahamu vema matunda na baraka ya hizo Sakramenti na hivyo basi hakutaka familia yake ikose baraka za Mungu.

Alihakikisha walijua sala zote za nyakati mbalimbali, alimtayarisha vema Yohane Bosko kwa sakramenti za Kanisa. Alimlea katika imani na maadili hadi kufikia wito wa upadre. Tuchukulie Yohane Bosko kipekee: alimfundisha kumsalimu Bikira Maria kila siku kwa sala ya ‘*Salamu Maria’*. Mama Margaret aliwafundisha watoto wake kuchukua majukumu ya familia hasa ya kazi za shambani. Katika hii familia watoto wengine walikuwa:- Joseph, Anthony na Teresa ambaye alifariki katika umri mdogo. Hivyo basi, ni wazi kuwa Mama Margaret alikuwa mama wa kipekee sana;- mama mwenye sala na imani thabiti moyoni, na pia mama mwenye huruma na uvumilivu moyoni. Alimtambua Mungu kuwa ndiye mlinzi na mfadhili wake. Familia ilipata pigo kuu wakati Fransisko Bosko alikufa. Ni wakati huu ambapo Yohane Bosko alikuwa tu na umri wa miaka miwili.

Majukumu yote ya familia yalimwangukia Mama Margaret Occhiena. Mama huyu alionja taabu ya kuwalea watoto bila baba,

alipiga moyo konde na kumwamini Mungu. Uwezo wake mkuu ulitokana katika imani thabiti ambayo alipokea kutoka kwa wazazi wake. Alitimiza wajibu wake na kumtumainia Mungu pekee. Yeye ni mfano bora wa mama ambaye anaelewa majukumu yake ya familia na pia majukumu ya imani yake.

## MAISHA YA MTAKATIFU YOHANE BOSKO

Yohane Melchior Bosko alizaliwa tarehe 16 Agosti 1815. Alizaliwa na kukulia katika jami na parokia ya *Castelnuovo d'Asti* nyakati hizi inaitwa *Castelnuovo* Don Bosco, katika kijiji cha *Becchi*. Baba yake aliitwa Francis Louis ambaye alikuwa hapo awali alioa na mkewe wa kwanza akafa, alikuwa na watoto wawili: Antoni na Teresa ambaye alifariki katika umri mdogo. Katika ndoa yake ya pili alimwoa Margaret Occhiena wa Serra Capriglio[ 1788-1856] na walikuwa na watoto wavulana Joseph[ 1813-1862] na Yohane[1815-1888]. Yohane alizaliwa 16 Agosti 1815 na akabatizwa siku iliyofuata katika Kanisa la Mt. Andrea na Padre Joseph Festa. Wasimamizi wake walikuwa Occhiena Melchior wa Capriglio na Magdalene Bosco wa Castelnuovo.

Familia yake Yohana Bosko ilikuwa maskini sana, walikuwa na shamba dogo, nyumba kiasi na bustani la mizabibu. Kwa kuiwezesha familia; baba Fransisko alimfanyia kazi mtu mmoja tajiri, shambani la mizabibu. Siku moja alirudi akiwa afya yake imezoroteka kwa kuugua. Bahati mbaya Fransisko alikufa 11 Mei, 1817 wakati Yohane alikuwa na umri wa miezi 21 karibia miaka miwili hivi. Yohana hakuelewa kuwa baba yake alikuwa amekufa, alidhani amelala tu na kwa nini haamki. Mama yake alimfahamisha kuwa hana baba tena na hatamwona katika ulimwengu huu.

Kifo cha Fransis kilikuwa pigo kubwa sana kwa familia; ilibidi mama yake Yohana Bosko, yaani Mama Margaret Occhiena, achukue majukumu yote ya familia. Mama huyu alikuwa mama wa sala, mnyenyekevu, mvumilivu na aliyewakaribisha maskini, japo walikuwa familia maskini iliyohangaika sana. Hakuweza kusoma na kuandika lakini alikariri mafundisho ya Kanisa na Katekismu moyoni mwake. Antoni yule mwana wa mke wa kwanza aliwahangaisha sana, hakua mtii. Mama Margaret alihuzunika sana kwa sababu Antoni alikuwa mtu mnyanyasaji, mwenye kiburi ambaye alimhangaisha Yohane Bosko katika umri mdogo alimtaka awe anafanya kazi zote za nyumbani na shambani. Antoni aliona kwenda shule ilikuwa kupoteza nafasi ya maendeleo katika familia.

**Ndoto katika umri wa miaka Tisa**

Wito wa Yohane Bosko waanza kujidhihirisha rasmi katika ndoto, ambayo inakuwa dira ya maisha yake yote. Yohane Bosko akiwa na umri wa miaka tisa, aliota ndoto ambayo ilimwongoza katika maisha yake yote. Katika ndoto alijipata akiwa katika uwanja. Na hapo kulikuwa na watoto waliocheza ambao walitumia lugha ya matusi. Yohane Bosko alijaribu kuwakanya kwa kupigana, waache kutumia lugha hiyo iliyowaelekeza katika dhambi bali hawakumsikiliza.

Mara mwanamume mmoja wa ajabu alijitokeza akamweleza Yohane Bosko, kuwa hataweza kuwaongoa hao vijana kwa vita au kupigana nao, bali katika upole na upendo watatambua uovu wa dhambi na kupenda wema na uadilifu. Hatimaye mwanamke wa ajabu na mzuri alitokea pia. Alimshika Yohane Bosko mkono kwa upole akamwonyesha kundi la wanyama wa mwituni waliogeuka na kuwa wanakondoo. Mama huyo alimwambia, "*Uwe mnyenyekevu, mvumilivu na mwenye nguvu*". "Yale unayoona yakiwatendekea wanyama hawa; nawe utawafanyia wanangu". Yohane Bosko alihisi kuwa Yesu na Bikira Maria wakimpa utume wa kutunza watoto na vijana walio katika shida. Yohane Bosko, alikuwa bado na hofu, hatimaye aliambiwa na yule mama, "*katika muda mwafaka utaelewa*". Baada ya Upadrisho alisali misa katika altare ya Bikira Maria Kanisa la Moyo Mtakatifu wa Yesu, huko Roma. Don Bosko alipatwa na furaha ambayo iliambatana na machozi kwa sababu aliielewa hiyo ndoto ya miaka tisa. Na alisema kuwa ni Bikira Maria aliyemfumbulia hayo.

**Maisha ya shule magumu**

Antoni hakupenda Yohane Bosko aende shule, alimtaka afanye kazi ya shamba pamoja na wao kwa sababu hakuelewa umuhimu wa kwenda shule. Hakuelewa nia ya Yohane Bosko ya kutaka kuwa padre. Katika umri mdogo Yohane Bosko aliwakusanya watoto wa umri wake, aliwasomea hadithi za kusisimua, aliwafanyia michezo ya sarakasi, kutembea juu ya kamba, mwishowe alisali sala ambayo mama yake alimfundisha - sala ya

‘*salamu Maria*’. Nia ya michezo yake ilikuwa ni kuwakusanya watoto na vijana ili kuwafundisha sala na maisha ya Mungu. Mama yake Margaret alimwandaa kwa Komunyo ya kwanza na tarehe 26 Mach 1826.

**Shamba la Moglia**

Kwa vile Antoni aliendelea kumsumbua sana Yohana Bosko, Mama Margaret alimhamisha Yohane Bosko hadi shamba la Moglia apate kazi huko na atoke katika usumbufu. Kila Jumapili aliweza kutembea kwa nusu saa kwenda Sakramenti ya kitubio huko *Moncucco*. Muungamishi wake alikuwa Padre Cottino alisikiliza kitubio chake. Kazi yake ilikuwa kuchunga ngombe au kazi zingine za shambani.

Katika umri mdogo aliweza kuwafundisha watoto wengine kumhusu Yesu. Akienda kuchunga ngombe alienda na kitabu cha Kilatini kujisomea kwa sababu, alisema kuwa anajiandaa kuwa padre. Kwa sababu ya kukosa baba katika umri mdogo, aliweza kupatwa na usumbufu wa namna mbalimbali na kukosa mtetezi. Kufuatana na maisha yake alianza kuelewa pia taabu na magumu ambazo ziliwapata vijana wengine.

**Maisha ya Seminari**

Cheri ndiyo Seminari, Yohane Bosko alipata nafasi ya kupata malezi na elimu ya kuwa padre. Mnamo tarehe 4 Novemba 1831, Yohane Bosko alingia Seminari iliyokuwa umbali wa kilomita 12 hadi *Castelnuovo*. Cheri ulikuwa mji wa wamonaki. Yohane Bosko aliweza kubaki huko miaka 10. Shuleni walisisitiza maisha ya Kikristo, misa kila siku, Sakramenti ya Kitubio, cheti cha tabia njema na kitabu cha sala. Yohane Bosko alisoma vizuri na alikuwa na kumbukumbu ya hali ya juu kimasomo.

**Malezi ya Upadre na Daraja ya Upadre**

Yohane Bosko alitafuta ushauri wa Padre Cafasso ambaye alikuwa baba wake wa kiroho. Padre Cafasso na Padre Cincano walimsaidia akaingia seminari ya jimbo mnamo tarehe 30 Oktoba 1835. Katika seminari aliweza kuacha kiamsha kinywa na

kukimbilia Kanisa la Mt. Philipo ili kupokea Ekaristi Takatifu. Mwaka 1841 alipata ushemasi. Alipadrishwa jumapili ya Utatu Mtakatifu Jumapili tarehe 5 Juni 1841 na Askofu Mkuu Fransoni. Baada ya kupata daraja la upadre Don Bosko alijiwekea malengo yafuatayo siku hiyo:

- *Kutumia muda wake vizuri;*
- *Kuwa na ukarimu kama wa Mt. Fransisko wa Sale;*
- *Masaa tano au sita kulala usiku na wakati wa mchana hamna kulala.*

Alisali misa yake ya kwanza katika sikukuu ya Utatu Mtakatifu, katika Kanisa la Mt. Fransisko wa Assisi, Torino katika altare ya malaika mlinzi. Siku hii ilikuwa kweli yenye furaha na ilikuwa sikukuu kabisa ambayo aliikumbuka miaka mingi.

**Utume kwa vijana**

Alitembelea katika njia za miji na akaona vijana wenye umri mbalimbali wakiwa wanajiingiza katika mambo ya utundu na maasi. Walikuwa wametoka sehemu mbalimbali za vijiji. Mwaka 1844, alishuhudia vijana 7148, wenye umri wa miaka 10 wakiwa wameajiriwa kwa kazi mbalimbali kama, ushonaji, wajenzi, wapaka rangi. Alitembelea magereza na akahuzunishwa sana kuwaona vijana wenye nguvu na akili umri kati ya miaka 12-18, wakiwa gerezani. Hali hii ilianza kumpa mawazo ya kutenda jambo la kuwasaidia hawa vijana.

**Mwanzo wa kazi kuu**

Tarehe 8 Desemba 1841, Sikukuu ya Maria Mkingiwa dhambi ya asili, katika Kanisa la Mt. Fransisko wa Assisi, akijiandaa kwa misa alimwona Comotti msakristia akimfukuza kijana mwenye umri wa miaka 16. Kijana huyu aliitwa Bartholomayo Garelli. Alifukuzwa kwa sababu hakujua kutumikia altareni. Baada ya Padre Yohane Bosko kumhoji, alipata kutambua kijana hakuwa amepokea Komunyo ya kwanza. Alianza kumfundisha Katekismu. Kwa kuona upole na upendo wa Padre Yohane Bosko; Bartholomayo alirudi Jumapili iliyofuata na vijana

wengine 6. Idadi ya vijana iliendelea kuongezeka na nafasi ilianza kuwa ndogo.
Ukarimu na upendo wa Padre Yohane Bosko, uliwavutia vijana wengi kwake. Na hasa sana ule uwepo wake kati yao. Alitumia muda mwingi mno kuwa kati ya hawa vijana. Vijana walimwona padre mwema, aliyewajalia kiroho na kimwili. Padre kuwa kati yao, ilileta usawa, hamna kijana alimdhulumu mwingine hata kidogo. Vijana walianza kukua kiroho na kimwili. Walifurahi kuwa miongoni mwa kundi kubwa lilokuwa karibu na padre.

**Nyumba ya Pinardi**
Baada ya kuhangaika sana, Padre Yohane Bosko alibahatika kupata sehemu ya shamba ambapo alianzisha oratori. Mnamo 22 Aprili 1846, Pasaka Jumapili; Askofu Mkuu alibariki hiki kiwanja. Vijana walipata nafasi ya misa, mafundisho ya dini, michezo, muziki na mengine mengi yaliwavutia vijana wengi. Wasaidizi mbalimbali walianza kujitokeza. Tarehe 3 November 1846, Mama Margareti alifika kuwasaidia vijana. Padre Yohane Bosko alijenga Kanisa dogo ambalo alisali misa pamoja na vijana. Hadi wa sasa kuna kikanisa kilijengwa ili kuweka huo ukumbusho. Kauli yake Mtakatifu Yohane Bosko ilikuwa kuwalea vijana ili wawe Wakristo wema na raia wema.

**Vyuo vya ufundi**
Bidii na sifa za Don Bosko zilienea Italia nzima. Alitenda miujiza mingi, alijenga makanisa, shule na vyuo vikuu, shule za ufundi kama useremala, uhunzi na kadhalika. Lakini kadiri sifa zake zilivyoenea vivyo hivyo ndivyo alivyopata maadui wengi. Wafitini na maadui wa dini Katoliki walimsumbua sana Don Bosko. Mara nyingi walimjaribu na kushindana naye juu ya dini, lakini hawakufua dafu mbele yake; walishindwa vibaya sana. Baadaye walikusudia kumua. Walimvizia mara kwa mara, lakini Mungu alimtuma mbwa mkubwa aliyeitwa Grijo ili amkinge mtakatifu wake na kuwafukuza maadui. Hata hiyvo Don Bosko hakujua mbwa huyo alitoka wapi. Maana alimfikia na kumwokoa wakati alipokuwa katika hatari.

Kazi zake zote Don Bosko, mfadhili wake alikuwa Mama wa Kristo. Alimletea msaada kwa namna mbalimbali. Watu wenye nia njema na wafadhili walifika kumsaidia katika kazi zake. Kazi zote zilifikia utimilifu. Na ulinzi na ufadhili huo bado aliukabidhi kwa kazi zake zote ulimwenguni. Mahali popote ambapo kuna jumuiya ya Mt. Yohane Bosko; pana ulinzi wa Bikira Maria na nguvu za Mungu. Ni imani iliyo kuu sana kujua na kuamini hayo yote.

**Shirika la Waselisiani wa Don Bosko**

Mwaka 1854 Don Bosko aliwaunganisha wasaidizi wake katika Shirika, ili kazi yake ya kuwaongoza na kuwalea vijana iendelezwe nao kwa kuwa alimthamini sana Mt. Fransisko wa Sale, wasaidizi hao wakaitwa Wasalesiani wa Don Bosko. Baadhi yao aliwatuma kama wamisionari kuhubiri injili katika nchi za Amerika ya Kusini, Afrika, China, Ujapani na visiwa vya Uhindi. Shirika la Waselisiani wa Don Bosko ni la kimataifa na ni la kimisionari.

**Shirika la Masista wa Maria, Msaada wa Wakristo**

Zaidi ya kuwaongoza wavulana, Don Bosko alielewa mahitaji ya wasichana. Hivyo mnamo mwaka 1872 akisaidiana na mama Maria Mazarello, alianzisha Shirika la mabinti, nalo huitwa Shirika la Mabinti wa Maria, Msaada wa Wakristo. Shirika hili ni kwa ajili ya kuwalea wasichana. Maria Mazarello alitangazwa kuwa Mtakatifu mwaka 1951. Don Bosko alifariki mwaka 31 Januari 1888 akiwa mzee mwenye miaka sabini na mitatu. Mwaka 1934 alitangazwa rasmi kuwa mtakatifu na msimamizi wa vijana. Kila mwaka Waselisiani hufanya Sikukuu ya huyo Mtakatifu kila tarehe 31 Januari.

**Vikundi vingine**

Katika familia ya Waselisiani wa Don Bosko kuna vikundi hivi pia: Waselisiani washiriki :- hawa ni wale waamini na watu mbalimbali ambao wanavutiwa na maisha ya Don Bosko, wanajiunga ili kuendesha karama ile  ya Don Bosko kama walei

kwa namna mbalimbali, aidha kuwa wafadhili wa kazi na utume wa waselesiani au kufundisha na kushiriki kazi zote. Wale wote waliosoma shule za Don Bosko na wale pia wamelelewa katika parokia za Don Bosko hao pia wana nafasi maalum katika shirika na wanashika nafasi ya kusaidia utume wa Don Bosko kwa hali na mali. Kikundi cha Maria Msaada wa Wakristo nacho, kinaeneza ibada kwa Ekaristi Takatifu na heshima kwa Mama Bikira Maria.

**Utakatifu wa Yohane Bosko**

Yohana Bosko alikuwa mtu aliyesali sana. Alikuwa na imani kuu kwa Mungu. Msingi wa wake wa utakatifu ulikuwa: - *upendo kwa Bikira Maria, Ibada kwa Yesu katika Ekaristi Takatifu, Elimu ya malezi kinga ambayo imejikita katika furaha na matumaini na Ibaada kwa Kanisa na heshima kwa Baba Mtakatifu*. Kwa ukarimu wake, Mungu alimpa yote katika wito wake. Mungu alimpa miujiza mingi na matendo makuu kwa ajili ya kudhihirisha utukufu wake. Aliweza kuwaponya watu wengi wakiwemo viziwi, viwete na wakati mmoja alimfufua kijana mmoja.

Alikuwa na uwezo wa kutabiri. Aliweza kutumia sala na imani kuu kwa Mungu kuwasaidia wahitaji. Aliwaeleza vijana wake kuwa mtakatifu mtu hauhiitaji mambo mengi ya ajabu, ni kutimiza wajibu wa kila siku hali umeungana na Mungu katika moyo wako. Aliwaeleza vijana wake wasifanye malipizi ya ajabu. Aliwaambia Waselesiani na vijana kuwa:- "*Mungu ataka sisi tuwe na furaha na kufurahia upendo wa Yesu*".

Don Bosko aliwaeleza kuwa, watimize wajibu wao, nyumbani, shuleni na majukumu mengine. Aliwaeleza wamtolee Mungu maisha yao hata nyakati za furaha na huzuni. Aliwafahamisha kuwa maisha yanatuletea nafasi nyingi kushiriki mateso ya Kristo: Kama hali ya hewa, kushindwa kufaulu jambo fulani, ugonjwa wa mwili, huzuni mambo haya yatakufanya mtakatifu. Katika shule ya Don Bosko kulitokea kijana mtakatifu aliyeitwa Dominiko Savio. Mt. Dominiko Savio kijana wa Don Bosko

aliaga akiwa na miaka 14, baadaye alitangazwa Mtakatifu. Huyu anatuonyesha utakatifu upo kwa ajili ya kila mmoja.

**Mafundisho kumhusu Mtakatifu Yohane Bosko**

Mtakatifu Yohane Bosko alikuwa mtu wa Mungu, rafiki wa Mungu maana mara zote alikuwa ameunganika na Mungu katika sala. Aliwaongoza wafuasi na vijana wake katika upendo wa Mungu. Alielewa kuwa wito wake ulikuwa zawadi kwa watoto na vijana na ndiposa, akaishi nadhiri ya utii, Useja na ufukara (*Obedience, Chastity* and *Poverty)*.

Yaani maisha yake ilikuwa kumpa Mungu utukufu wake kwa kuwalea vijana katika imani, kazi na furaha. Mtakatifu Yohane Bosko ni mwalimu kwa sababu yeye alielewa kumkomboa mwanadamu ni kumpa elimu kuanzia umri mdogo. Kumpa kijana uhai ni kumfundisha kumjua Mungu, kumtii na kumtumikia katika talanta na ujuzi wa maisha. Mtakatifu Yohane Bosko ni baba wa vijana kwa sababu aliwalea vijana wake kwa maadili, aliwatakia mema na walimwona nyakati nyingi akiwa pamoja nao; katika michezo, masomo, sala na kazi. Mtakatifu Yohane Bosko alikuwa rafiki wa Mungu kwa sababu ya mambo muhimu aliyoweka mkazo:

- *Upendo kwa Maria Msaada wa Wakristo;*
- *Ibada kwa Yesu katika Ekaristi Takatifu;*
- *Mtindo wa elimu, furaha na matumaini;*
- *Utii na upendo kwa Kanisa la Yesu Kristo.*

Kazi na utume wa Don Bosko bado unadhihirika hapa ulimwenguni na hasa katika Afrika mashariki kuna shughuli nyingi za utume wa Don Bosko.

Oratori

Mwaka 1840 kando mwa mji wa Torino kulikuwa watu maskini sana, vijana na watoto waliokuwa wakichukuliwa kufanya kazi viwandani. Yohane Bosko alitambua utume wake ulikuwa hapo. Alitembelea magereza na Padre Cafasso ambaye alikuwa baba wake wa kiroho. Kwa kuwasaidia hawa vijana bila senti lakini

kwa imani kwa Bikira Maria alianzaisha Oratori. Oratori ilikuwa sehemu ya sala na pia ya burudani, ambapo vijana walikusanyika kila Jumapili. Sehemu hii ilikuwa aidha parokiani, shuleni au uwanja ulio wazi. Don Bosko aliwafundisha vijana na watoto: Katekismu, sala, Neno la Mungu na aliwapa pia nafasi ya kucheza michezo mbalimbali na hatimaye kuwapa wazo njema kabla hawajatawanyika. Mwanzoni Don Bosko alipata sana shida kuendeleza utume wake wa Oratori, hakuwa na sehemu maalum bali alikuwa akihamahama. Alikuwa anakutana na hawa vijana kila juma.

Oratori ya Mt. Yohane Bosko ilikuwa na madhumuni manne muhimu. Alitaka Oratori yake kuwa shule, sehemu ya michezo, sala na nyumbani kwa vijana na watoto. Hizo sehemu zote zilikuwa muhimu kwa makuzi ya watoto na vijana. Ilikuwa ni nafasi ya kumsaidia kijana kukua mkamilifu. Kama alimwona kijana Kanisani tu pekee na katika michezo haonekani alijua kuna hali yake haikuwa nzuri. Kama kijana alionekana hana ushirika na wenzake alitafuta kujua ni kwa nini. Kama kijana alipendelea tu kujisomea na hana ushirika na wengine, angelijitahidi kumsaidia kujifunza kuishi vema na wengine. Zile sehemu nne za vijana muhimu kwa makuzi yao ni kama ifuatavyo:

- **Nyumbani** – *Sehemu ambayo kijana anajisikia nyumbani, huru sana na salama.*
- **Shule** – *Sehemu ya kuelimika ambayo inamletea kijana maarifa, mambo mapya ya kumpa matumaini*
- **Kanisa** – *Sehemu ya kuelewa maisha na kukua kiroho, kumfahamu na kumjua Mungu.*
- **Uwanja wa michezo** – *sehemu ya burudani*, kukuza vipaji, kufurahi na pia kujifunza kushirikiana na wengine.

Kama wazazi, vijana, marafiki na walimu wakielewa maneno hayo manne hapo juu, basi ni rahisi sana kuelewa kwa kiundani karama ya Mt. Yohane Bosko. Huyo Yohane Bosko alielewa kuwa vijana walitaka kujisikia nyumbani, sehemu ambayo

wanakaribishwa na kukubalika. Wakati vijana wanajisikia salama na furaha, ni rahisi kwao kujenga imani na pia makuzi mazuri. Watakuwa na uhuru wa kueleza mawazo yao na hisia zao. Vijana wakikosa ile hali ya kuwa wazi na kujisikia salama, basi watafunga mioyo yao kwa sababu watatawaliwa na woga.

Kama mazingira ya Mt. Yohane Bosko yalikuwa sehemu ya shule na elimu, basi tukumbuke kwamba ilikuwa ni njia mojawapo ya kuwaondoa vijana toka umaskini. Shule na elimu kwa Mt. Yohane Bosko ilikuwa ule upendo moyoni wa kumwona akiwa na furaha na matumaini. Kama vijana wanaushirikiano mwema basi wataweza kujifunza mambo ya msingi ya maisha, kama kujitambua wao ni nani, wana talanta zipi, mapungufu yao. Hivyo Basi Mt. Yohane Bosko aliweza kufanya kila hali ya kujielimisha kwa kijana: michezo, kazi, ushauri, mahangaiko na shida mbalimbali. Alitamani sana katika kila oratori wakati vijana wamekusanyika kuwepo na Msalesiani au mlezi au mwalimu au mzazi ambaye atawasaidia kwa kirafiki vijana wajitambue.

Katika michezo vijana na watoto wapaswa kuweka bidii na nguvu zao katika michezo, mazoezi. Mt. Yohane Bosko alitambua kuwa waelimishi wengine walifikiri kuwa ilikuwa kupoteza wakati kuwa kati ya vijana. Mt. Yohane Bosko alielewa michezo kuwa sehemu maalum kwa kijana, kwa sababu ilikuwa aina moja ya kusherehekea maisha. Umuhimu wa michezo na shughuli za kawaida huonekana kuwa si jukumu ngumu. Hivyo basi inafanyika kwa njia ya upendo na furaha na inatuwezesha kutumia muda vizuri.

Mt. Yohane Bosko alithamini sana michezo na shughuli za kawaida zilizompa kijana nafasi ya kucheza na kufurahi hivyo, kumpa nafasi ya kukua kimwili na kiroho. Nia ya Mt. Yohane Bosko kuweka Oratori zake karibu na eneo la Kanisa ilikuwa kushirikisha imani na furaha kama sehemu ya makuzi. Mt. Yohane Bosko alitaka kila hali itambulike uwepo wa Mungu. Aliweka kanisa wazi kila siku mpaka jioni. Aliwashauri wote kwenda ndani ya Kanisa mara kwa mara hata wakati wa michezo au wakati wa mapumziko. Ndivyo ilivyo desturi katika vyuo na

shule zote za Mtakatifu Yohane Bosko, wote wanashauriwa kutembelea kanisa na kusali kwa muda mfupi hata ingebidii mara nyingi, kuwakumbusha uwepo wa Mungu.
Oratori ndio maisha ya Waselesiani wa Don Bosko mahali popote walipo. Hapa Afrika Mashariki na sehemu zingine Afrika na ulimwenguni kote, utakuta watoto na vijana wakiwa wengi katika vituo vya Don Bosko. Utapata maisha ya oratori kadiri ilivyoelezwa hapo juu. Hapa Afrika Mashariki oratori huwa sehemu kijana wowote hapendi kukosa, maana ndipo mahali hupata furaha. Wengi waliopata nafasi ya maisha hayo ya Oratori huwa na kumbukumbu njeam zaidi. Hasa hapa Kenya oratori zinawapa watoto nafasi ya kukutana na Waselesiani na marafiki wa Don Bosko kutoka mataifa mbalimbali. Moyo wa Oratori ni kuwa, wote hujisikia nyumbani na pia katika familia moja. Japo wengi huvutiwa na michezo pamoja na burudani lakini, hukua katika hali zote za kiroho na kimwili.
Katika oratori, vijana na watoto huonja upendo wa mchungaji mwema. Huwa kuna mapadre au masista au mwalimu au Waselesiani washiriki, ambao kwa uwepo wao huwa alama ya usalama. Ni watu ambao watawapa mawaidha na pia kuwapa ulinzi endapo watajisikia wanahitaji lolote. Kwa hivyo watoto na vijana huwa na furaha na uhuru kwa sababu wanajisikia furaha kuwa kuna watu ambao watawakimbilia kwa hitaji lolote. Hii ndiyo alama ya mchungaji mwema kati ya watoto na vijana. Ukitaka kujua hali ya oratori tembelea vituo vya Waselesiani hapa Kenya na sehemu zingine za Afrika.
Katika oratori, tulitambua maisha ya Waselesiani wa Don Bosko: mapadre, mabruda, masista na wasaidizi wengine. Watoto na vijana wanapofika katika sehemu hizo wanakutana na makaribisho ya furaha. Ni wao wa kwanza kukufikia na kukusalimia na pia kukuuliza hali yako na kukupa neno la kukupa matumaini. Unajisikia upo nyumbani na pia waweza kujifunua hali yako ya roho na kusema shida ambayo ina kukera, iwe ya familia yenu au kawaida. Katika oratori, katika umri mdogo watoto na vijana hukuza vipaji mbalimbali, kama vya michezo,

muziki na sana sana, utakuja kukuza paji la sala. Ni hapo utaelewa maana ya Ekaristi Takatifu, utasikia habari ya Mungu, utawajua maisha ya watakatifu wengi na zaidi utajifunza kuwa mkristo mwema na raia mwema, kwa sababu unajifunza kuishi na wengine katika michezo mbalimbali. Na hapo ndipo unajenga utu, urafiki na hali ya moyo mwema.

Wazazi na walimu, wakielewa maana ya oratori na kuwapa watoto wao, mafanikio huwa makubwa sana hasa katika masomo. Kwa sababu oratori huleta nidhamu ndani ya kijana na watoto pasipo kutumia ukali na adhabu bali upole na maelekezo mema. Hali hiyo umfanya mtoto kupenda elimu na imani, mambo ambayo yanampa makuzi mazuri. Watoto na vijana hujisikia watu maalum, na hivyo hujenga mawazo mazuri na tabia njema. Waselesiani wa Don Bosko wapaswa kusambaa Kenya yote ili watoto na vijana wapate nafasi katika karama hii ya Mtakatifu Don Bosko. Kilele cha mambo yote, ni kukuza miito. Vijana na watoto wengi huvutiwa na miito mitakatifu kwa hali ya wanayoona katika oratori.

**Mtindo wa Malezi Kinga wa Mtakatifu Yohane Bosko**

Mtakatifu Yohane Bosco ambaye hujulikana kama Don Bosco, Kanisa lamtambua kuwa Baba na mwalimu wa vijana. Ajabu ni kwamba katika historia ya maisha yake, Yohane Bosco alifiwa na baba yake akiwa mdogo sana wa miaka miwili tu , mama yake hakuwa na uwezo wa kumpeleka shuleni . Misaada ya wenye huruma na juhudi zake mwenyewe ndizo zilimwezesha kumaliza masomo yake. Alijenga maisha yake katika ukarimu wa watu wengine.

Akiwa Padre kijana, alikabiliana na vijana waliokuwa wakimiminika katika mji wa Torino, Italia kaskazini, kutafuta masilahi yao. Hali ilvyokuwa enzi hizo si tofauti sana na sasa huku kwetu, vijana hawakupewa fursa ya kufanya lolote halali. Hivyo Don Bosko alisikitishwa sana na hali ya vijana wengi kuingia gerezani kwa sababu ya makosa mbalimbali. Upotovu wa vijana ulizidi , na kwa kuwa walikuwa wengi waliomiminika mjini, mabepari na wowote wanaotaka kujinufaisha kutokana na

hali hiyo, waliwanyanyasa vijana. Don Bosko alizoea kuzuru katika magereza mbalimbali pamoja na Padre mwenzake aliyeitwa Joseph Cafasso. Kuona hali jinsi ilivyo kuwa Don Bosco alijiuliza swali, ni tendo lipi laweza kufanyika ili vijana wasiingie gerezani?

Swali hilo lilimfanya Don Bosko kubuni mbinu za kuwasaidia vijana wasiingie gerezani. Hayo ndiyo yaliyokuwa mapendo ya Don Bosko kwa vijana hawa wa mitaani ili wasiingie gerezani tena. Alianzisha mtindo wa elimu wa kulea vijana ambao unahusu: kuzuia kuliko kuponya, akauita elimu malezi kinga (*Preventive system of Education*)

**Mambo Muhimu ya Mtindo huu na kwa nini yafaa yatumiwe**

Kwa kawaida kuna mitindo miwili ya malezi ambayo imekuwa ikitumika kote mpaka sasa. Kuna mtindo wa kuzuia maovu yasimpate kijana (*Preventive*) na ule wa kukandamiza kijana au kumfunga asitende maovu (*repressive system*). Mitindo hii huwafanya vijana wasitende maovu au wasipotoke, kinachofanywa kwanza ni kutunga sheria zinazokataza mambo fulani. Mtindo wa (*repressive*) hutawaliwa na yafuatayo:

1. *Kuzifanya sheria zijulikane kwa wote.*
2. *Kuchunguza anayezivunja sheria hizo.*
3. *Na mwisho kuwaadhibu wavunjao sheria ili mambo hayo yasirudiwe tena.*

Mtindo huo hapa juu ni kinyume kabisa katika malezi ya mtoto au kijana. Elimu ya malezi kinga (*preventive*) yahitaji sheria zitungwe pia na zijulikane kwa wote wanaohusika. Katika mtindo huu, mkuu au Gombera na wasaidizi wake ni lazima wawe miongoni mwa vijana na wanafunzi ili vijana wakumbushwe yawafaayo kufanya na vijana wasipate nafasi ya kutenda jambo mbaya, mfano kutusiana, kugombana au kupigana.

Walezi wapaswa kuwa miongoni mwa watoto na vijana si kama polisi au watu wenye kutiisha amri kwa uwezo wao, bali wawe kama wazazi, ndugu, rafiki, wenye kutoa msaada ukihitajika .

Watazungumza na watacheza nao, kuimba nao na hata kutembea nao, mradi wawe tayari kila mara kuwaonyesha watoto na vijana yanayoweza kuwapata ili vijana yasiwashawishi kutenda kosa au dhambi. Sehemu hizo ni Kanisa, bwaloni, michezoni, kazini na darasani na wakati wa mapumziko.

**Msingi wa mtindo wa kuzuia maovu (*preventive system*) ni :**

1. *uwezo wa kutoa na kutambua sababu.*
2. *Imani thabiti katika misingi ya dini - Katoliki*
3. *Moyo na vitendo vya mapendo.*

**Mtindo huu wa malezi unafaa kwa sababu zifuatazo:**

*Kwa kijana aliye na habari ya namna ya mtindo huo unavyo fanya kazi, hakati tamaa upesi kama akianguka katika makosa au dhambi.*

1. *Watoto Ni watukutu tena hawaoni mbali katika mawazo yao, kidogo tu wamesahau umuhimu wa sheria hii na adhabu au maonyo yawezayo kufuatia.*
2. *Ule mtindo wa (repressive) wa malezi , amri kali ya kuzuia vijana wasifanye makosa unaweza kufanya nidhamu ya mahali , lakini hauwasaidii wahusika kuwa watoto na vijana bora zaidi .*
3. *Kwa mtindo wa kinga maovu ,vijana wanaelewa zaidi sababu hii au ile ,anenalo kwa lugha ya moyo wakati wakiwa shuleni au hata katika maisha yao ya baadaye.*

Kauli yake Mtakatifu Yohane Bosko ilikuwa kuwalea vijana ili wawe Wakristo wema na raia wema. Na katika hali ya malezi huo ndio mtindo bora ambao huyo mtakatifu alitumia kwa miaka mingi kwa ajili ya kuwaokoa vijana. Alitembelea hata magereza na kuwaongoa vijana.

# FAMILIA YA BIKIRA MARIA

## Familia ya Bikira Maria

Kumfahamu Bikira Maria ni vema kuanza na familia yake. Kutokana na mapokeo ya zamani karibu karne ya pili tunafahamu kuwa Yoakimu na Anna ndio wazazi wa Bikira Maria. Yoakimu alitokea katika kabila la Yuda na ukoo wa Daudi. Naye Anna mkewe alizaliwa katika ukoo wa Haruni, kuhani Mkuu. Katika maandiko ya Mt. Yeronimo anatueleza ya kuwa; hawa wazazi wawili waligawa mali yao mafungu matatu: *fungu moja lilitumiwa kwa kupamba hekalu la Yerusalemu*; *fungu jingine waliwagawia maskini*; na *fungu la tatu walilihifadhi kwa chakula chao wenyewe*. Ukarimu huo wao ni ishara ya utakatifu uliokuwa mioyoni mwao. Mazingira yao yalikuwa matakatifu sana, ndipo Mungu aliwateua wawe wazazi wa Bikira Maria. Hivi ndivyo familia zapaswa kuwa chemichemi za wito.
Tangu zamani karne ya sita Wakristu walizoee kuwaheshimu wazazi hao. Mt. Yohani wa Damasko aliwasifu akisema: "*Tunawatambua ninyi wawili kutokana na mtoto mliyemzaa*". Bikira Maria asiye na doa aliweza kuzaliwa tu na wazazi wenye moyo safi, na mama wa Mungu sharti azaliwe na wazazi waliokuwa marafiki wa Mungu. Kama katika familia watu watasali kwa bidii basi hayo yanakuwa makao ya Mungu. Na ni dhihirisho kuwa familia zote zimo katika mpango wa Mungu.

## Kuzaliwa Bikira Maria

Tarehe 8 Desemba tunasherehekea sikuu ya Bikira Maria mkingiwa dhambi ya asili. Sherehe hii ni ya Maria imakulata maana yake "**asiye na doa**". Tangu zamani za kale Wakristu wengi wamesadiki kwamba Maria alikingiwa dhambi ya asili. Mungu alimwuumba Bikira Maria, na tangu milele alikuwa amemchagua awe Mama yake. Ukweli unaokumbukwa ni kwamba, Maria tofauti na watu wengine wote, hakurithii dhambi ya asili wala hakutenda dhambi yo yote kwa hiari yake alipoweza kuchagua kati ya jema na baya.

Hivyo tangu mwanzo wake, alipokuwamo bado tumboni mwa Mamae Anna, Maria alikuwa Mtakatifu sana akimwelekea Mungu tu. Mara Maria alipotungwa tumboni mwa Mamae, Mungu aliijaza roho yake neema ya utakaso, na hivyo Maria hakujua kabisa tamaa mbaya inayomvuta mtu atende dhambi. Hali hiyo nzuri iliwezekana kwa ajili ya mastahili ya kifo chake Yesu Kristo ambaye Maria aliwahi kushirikishwa hata kabla ya Yesu hajazaliwa bado. Hivyo ni wazi, kwamba kama vile wanadamu wote, Maria naye aliokolewa na Mwanae Yesu aliye Mwokozi wa watu wote kabisa.

Fundisho hilo lilitangazwa kuwa nguzo ya imani yetu ya Kikatoliki mnamo tarehe 8 Desemba 1854 na Papa Pius IX katika barua yake *ineffabilis Deus*. Miaka minne baada ya mwaka 1858, Bikira Maria alimtokea Bernadetta wa Lurdi, naye alimuuliza mwanamke mzuri aliyemwona kwenye pango kilimani, “unaitwaje”? Maria alikunjua mikono yake akaiinua juu akaifunga tena, akasema: “*Mimi ndimi mkingiwa Dhambi ya Asili*”.

Bikira Maria alikuwa binti wa Israeli, msichana wa Kiyahudi wa Nazareti na Galilaya. Kumchagua Bikira Maria tangu milele; ni upendo wa Mungu kwa wanadamu wote. Katika Injili ya [*Yohane 3:16],* tunasoma, “ *kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye awe na uzima wa milele*”. Mungu alimtayarishia mwili, alitaka ushirikiano huru wa kiumbe. Mungu alipata ushirikiano huo kutoka kwa Bikira Maria katika uhuru wa imani. Maana yake kumchagua Mungu pekee na kufuata mwito wake. Basi Mungu wa milele alimchagua Bikira Maria awe Mama wa Mwanawe. Mungu alimtuma Mwanawe, lakini kwa ajili ya kumtayarishia mwili, alitaka ushirikiano huru wa kiumbe. Kwa ajili hiyo, Mungu wa milele yote alimchagua Bikira Maria awe mama wa Mwanawe binti wa Israeli, msichana wa Kiyahudi wa Nazareti ya Galilaya.

**Kukingiwa dhambi ya Asili**

Kwa ajili ya kuwa Mama wa Mkombozi, Bikira Maria alitajirishwa na Mungu kwa karama nyingi zenye kulingana na kazi iliyo kubwa hivi. Malaika Gabrieli wakati wa kupasha habari alimsalimu kama “**aliye jaa neema**”. Kwa kweli, aweza kutoa kibali huru cha imani kwa habari ya wito wake, ilikuwa lazima maisha yote awe amejaa neema ya Mungu. Zaidi ya mtu ye yote yule aliyeumbwa, Baba **“alimbariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo”** na akamchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili awe mtakatifu na bila hatia mbele zake katika pendo.

Wakati wa kupashwa habari kwamba angemzaa “**Mwana wa aliye juu**” bila kumjua mwanamume, kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, Maria alijibu kwa utii wa imani: akiwa na hakika kwamba “**hakuna lisilowezekana kwa Mungu**”. “**Mimi ni mjakazi wa Bwana; na iwe kwangu kama ulivyosema”**. Kwa kukubali Neno la Mungu, Maria amekuwa Mama wa Yesu, akikumbatia kwa roho yake yote, bila kushikwa na dhambi yoyote, mapenzi ya Mungu ya Wokovu, na alijitoa kabisa kwa nafsi yake kwa kazi ya Mwanawe ili kuhudumia fumbo la ukombozi chini yake na pamoja naye na kwa msaada wa neema ya Mungu.

**Umama wa Bikira Maria**

Wanadamu wote huingia hapa duniani kwa njia ya Mama, ambaye amepewa nafasi ya pekee na Mungu, kupokea mbegu ya kiume na kuirutubisha katika tumboni mwake. Kwa baraka zake Mungu mama anashiriki uumbaji wake. Na mtoto hutunzwa na mama sana hadi mtu mzima. Bikira Maria naye ni Mama wa Mwokozi si kwa njia kama vile ya kibinadamu bali ya Mungu, kama vile tunavyoelezwa hapa chini:

*Umama wa Bikira Maria umo ndani ya mpango wa Mungu. Ubikira wa Maria wadhihirisha hatua ya kwanza kabisa ya Mungu katika Umwilisho. Yesu ni Mungu tu kama Baba. Asilii ya kibinadamu ambayo ameitwaa haikumtenga kamwe na Baba;*

*kwa asili ni Mwana wa Baba kadiri ya uungu ; kwa asili ni Mwana wa mama kadiri ya ubinadamu, lakini Mwana halisi wa Mungu katika hali hizo mbili.*
*Maria ni bikira kwa sababu ubikira wake ni alama ya imani yake, ambayo haikubadilishwa na shaka lolote, na ni alama ya kujitoa kwake kabisa kwa utashi wa Mungu. Kwa imani ni mama wa Mwokozi: "Maria ana heri zaidi kupokea imani ya Kristo kuliko kutungwa mwili wa Kristo. Maria ni bikira na mama wa pamoja kwa sababu yeye ni ishara na utimilifu wa Kanisa: " Hakika Kanisa…kwa kupokea Neno la Mungu kiaminifu, linakuwa pia mama, kwani kwa mahubiri na ubatizo linazaa watoto waliotungwa na Roho Mtakatifu na kuzaliwa na Mungu kwa uzima mpya usiokufa. Ni bikira pia anayetunza imani yote na safi, aliyompa mchumba wake.*

**Bikira Maria amejaa Neema**
Maria, Mtakatifu kabisa, Mama wa Mungu, Bikira daima ni kilele cha utume wa Mwana na wa Roho Mtakatifu katika utimilifu wa nyakati. Kwa mara ya kwanza katika mpango wa wokovu na kwa sababu ya Roho wake amemtayarisha, Baba apata "*makao*" ambamo Mwana wake na Roho wake wanaweza kukaa kati ya watu. Kwa maana hii mapokeo ya Kanisa yamesoma mara nyingi, kuhusiana na Maria, matini, yaliyo bora sana juu ya hekima. Maria anaimbwa na kuwakilishwa katika liturjia kama "*kiti cha Hekima*". Ndani yake, "maajabu ya Mungu" ambayo Roho atayatimiza katika Kristo na katika Kanisa yanaanza kujionyesha.
Roho Mtakatifu, alimtayarisha Maria kwa neema yake: Ilifaa Mama wa yule ambamo "*unakaa utimilifu wote wa Mungu kwa jinsi ya Kimwili*," awe "*amejaa neema*." Kwa neema tu alichukua mimba bila dhambi kama kiumbe aliye mnyenyekevu, na aliyeweza sana kupokea zawadi ya Mwenyezi isiyoelezeka. Kwa heshima ya haki Malaika Gabrieli amsalimu kama Sayuni: '*ufurahi*'. Ni shukrani za taifa lote la Mungu, na kwa wimbo wake, akiwa amechukua ndani yake Mwana wa milele. Ndani ya Maria, Roho Mtakatifu anatekeleza mpango wa Baba uliojaa upendo. Kwa njia ya Roho Mtakatifu, Bikira alipata mimba na

kumzaaa Mwana wa Mungu. Ubikira wake unakuwa uzazi wa pekee kwa uwezo wa Roho Mtakatifu na kwa imani.
Katika Maria, Roho Mtakatifu anamdhihirisha Mwana wa Baba aliyefanyika Mwana wa Bikira. Yeye ni kichaka kiwakacho cha tokeo halisi la unyenyekevu wa mwili wake na anamfanya ajulikane kwa maskini na kwa matunda ya kwanza ya mataifa. Kwa njia ya Maria, Roho Mtakatifu anaanza kuwaweka watu katika ushirika pamoja na Kristo ambao ndio lengo la pendo la huruma ya Mungu. Wanyenyekevu ndio wa kwanza kumpokea: wachungaji, Mamajusi, Simeoni na Anna, wana-arusi wa Kana na wafuasi wa kwanza.
Katika kilele cha utume wa Roho Mtakatifu, Maria anakuwa ndiye "**Mwanamke**," **Eva Mpya** (*Mama wa walio hai*"), Mama wa "Kristo mzima". Na kwa namna hiyo yuko pamoja na wale Thenashara, "wakidumu kwa moyo mmoja katika kusali," alfajiri ya nyakati za mwisho" ambapo Roho ataanzisha asubuhi ya Pentekoste kwa udhihirisho wa Kanisa.

**Maria Mama wa Yesu kwa uwezo wa Roho Mtakatifu**
Malaika aliwatangazia watu wachungaji kwamba Yesu atazaliwa, kama masiha waliyeahidiwa Waisraeli.
"*Leo Katika mji wa Daudi amezaliwa kwa ajili yenu Mwokozi, ndiye Kristo Bwana*"[ *Lk 2:11*]. Tangu Mwanzo Yeye ni "*Yule ambaye Bwana alimtakasa na kumtuma ulimwenguni*" aliyetungwa mimba kama "Mtakatifu" katika tumbo la Bikira Maria [*Yoh 10:36; Lk 1:35*]. Yosefu aliitwa na Mungu " Umchukue Maria mkeo, maana mimba yake ni kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, " ili Yesu aiitwaye "Kristo" azaliwe na mchumba wa Yosefu katika ukoo wa kimasiha wa Daudi[ *Mt 1:20; Mt 1:16; Rom 1:1; 2 Tim 2:8; Ufu 22:16*]

**Mwana wa Mungu amefanyika Mtu**
Katika imani ya Nikea – Konstantinopoli, tunaungama" Kwa ajili yetu sisi wanadamu na kwa ajili ya wokovu wetu" alishuka toka mbinguni; akapata mwili kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, kwake Yeye Bikira Maria akawa Mwanadamu.

***Neno alifanyika mwili:***

- Kwa ajili ya kutuokoa na kutupatanisha na Mungu: " ni Mungu aliyetupenda sisi, akamtuma Mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu, " Baba amemtuma Mwana kuwa Mwokozi wa ulimwengu " Yeye alidhihirishwa ili aziondoe dhambi"[ Yoh 4:10k 4:14; 3:5].
- Ili tujue pendo la Mungu. Pendo la Mungu lilionekana kwetu, kwamba Mungu amemtuma Mwanawe pekee ulimwenguni ili tupate uzima kwa yeye [1 Yoh 4:9]. " Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa Milele"[ Yoh 3:16]
- Ili tuwe washiriki wa tabia ya uungu. Ndiyo sababu ya Neno kufanyika Mtu, Na Mwana wa Mungu, amekuwa Mwana wa mtu Ili mwanadamu, kwa kuingia ushirika na Neno, na kwa kupata uana wa Mungu, awe mwana wa Mungu.

## BIKIRA MARIA KATIKA MAANDIKO MATAKATIFU

### Agano la Kale

Bikira Maria Mtakatifu sana, ni yeye aliyeandikwa katika Maandiko Matakatifu kuanzia Agano la Kale hadi Agano Jipya. Maandiko Matakatifu yanatuthibitishia halali ya kuwa Mungu kamjalia neema kuliko kiumbe chochote kuwa Mama wa Mwanaye. Ni mpango wa Mungu ambao unaonekana wazi kabisa kuwa huyu Bikira awe njia ya chemichemi ya baraka za ulimwengu kwa wanadamu wote.

Tunaelezwa katika Agano la Kale kuwa Maria anaonekana tayari katika utabiri wa kinabi katika ahadi ya kushinda joko aliyewashawishi Adamu na Eva kuingia katika dhambi [*Mwa 3:15*]. Maria pia anaonyeshwa kuwa bikira ambaye atamzaa mtoto, ambaye jina lake ataitwa Emmanuel [*Is 8:14*; *Mika 5:2-3*]. Katika injili pacha na matendo ya mitume ndimo jina Maria linapatikana.

**Agano Jipya**

Katika Injili ya Yohane, Bikira Maria anaitwa "*Mama wa Yesu*" au "*Mama yake*" [*Yoh 2:1, 3, 5, 12; 19:25-26*]. Maria ametajwa pia katika katika nyaraka za Mtume Paulo tunapata kutoka [*Gal 4:4*]"*Mungu alimtuma mwanawe azaliwe na mwanamke*…". Katika injili ya Luka Maria anasalimiwa na Malaika Gabriel kama yule ambaye amependelewa na Mungu [*Lk 1:28, 30*]. Yeye ni mjakazi wa Bwana [*Lk 1:38*]. Elizabeti anamwita "*Mama wa Bwana*"[*Lk 1:43*]. Yeye ni mwaminifu katika kusikia na kutenda Neno la Mungu. Maria anakuwepo wakati Yesu anaposulubiwa [*Yoh 19.25-27*]. Ni katika msalaba Yesu alimtolea mfuasi wake ambaye alimpenda sana kwa mama kama mwanawe na Maria kwa mfuasi kama mama. Hii ni ishara ya mwanzo wa Jumuiya ya wafuasi wanaoamini. Nyakati hizi , hiyo jumuiya ni Kanisa la Kikristo na wale wote wanao mwamini Yesu Kristo.

Kuwa Mama wa Mungu ni jambo kubwa sana, lisilo kifani. Kwa hiyo ilimpasa Maria aandaliwe kwa namna ya pekee kabisa. Kwa ajili hiyo, Mungu alimjaza Maria neema nyingi [*Lk 1:28*], na akamkingia dhambi ya asili tangu nukta alipotungwa mimba tumboni mwa mama yake Anna. Yeye ambaye angemzaa Bwana na Mkombozi wa ulimwengu, kwa mastahili ya Kristu, hakupaswa kuwa na doa lolote la dhambi. Kwa sababu ya Umwilisho wake, Yesu ni Mungu-Mtu.

Katika Nafsi Moja ya Yesu Kristu kuna hali zote mbili-hali ya kimungu na hali ya kibinadamu pasipo kutengana. Kwa kuwa Maria alipata Mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, anastahili kuitwa "*Bikir*a" au "*Bikira daima*". Hii ni imani ya Kanisa, ambayo limeungama nyakati zote. Tendo hilo la Mungu ni la ajabu sana, ambalo hekima ya mwanadamu haiwezi kung'amua bila hekima ya Mungu.

Maria alibaki kuwa Bikira kabla ya wakati na baada ya kumza Yesu. Alikuwa Bikira kabla ya kumzaa Yesu kwa sababu alipata mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Alikuwa Bikira wakati wa kumzaa kwa sababu alijifungua bila kuharibu ubikira wake. Maria alibaki kuwa Bikira baada ya kumzaa Yesu kwa sababu aliendelea kuishi na Yosefu kama kaka na dada na hakuwa na

watoto wengine. Bikira Maria, kujawa neema za Mungu ndivyo alikuwa chombo safi kwa ajili ya umama wa kiroho kwa wote wanaomwamini Mungu. Mungu alipenda tujisikie ulinzi wake na upendo kwa hali ya kibinadamu ambayo aliifanya ya kimungu. Na ndipo sasa wanadamu wote wamejenga tumaini kubwa kwa Mungu, Mungu anayewajali na kuwatunza katika hali wanayoiona, hisi na pia kuigusa.

Ndugu zake Yesu wanaotajwa katika Injili [*Mk 3:31; 6:3*], ni jamaa tu wa karibu, na siyo wa tumbo moja. Katika lugha ya *Kiebrania* na *Kiaramayo,* jamaa wote wanaitwa ndugu, iwe wa tumbo moja au sivyo. Hakuna hata sehemu moja katika Maandiko Matakatifu inaposemwa kwamba Maria alikuwa na watoto wengine zaidi ya Yesu. Kuna vidokeza kadhaa vinavyoonyesha kuwa Yesu alikuwa Mwana pekee wa Maria [*Lk 2; 46-52; Yoh 19:26-27*]. Msalabani Yesu alimkabidhi Mama yake kwa Yohane. Kama Maria angekuwa na watoto wengine, lisingekuwa jambo la busara kwa Yesu kumkabidhi mamaye kwa mtu wa pembeni na kuwaacha ndugu zake wa tumbo moja.

Ubikira wa Maria kitheolojia unaonyesha kwanza fumbo la harusi ambapo Mungu ni bwana arusi. Ubikira ni kuishi na moyo wa ibada makini kwa Mungu na Mwanaye. Na huu ndio mwito wa Mungu kwetu sisi wanadamu. Tumepewa Bikira Maria ishara ya kweli ya utii kwa Mungu. Mungu anayewapenda wanadamu upeo, na kila mara ataka kuwafanyia jambo nzuri. Ili neema za Mungu ziwafaidi wanadamu, wapata kuwa na mioyo wazi na utii kwa Mungu, kama vile Bikira Maria alivyokuwa. Na ni njia rahisi sana, kuishi na wazo la kumwamini Mungu katika roho yako.

## MAFUNDISHO YA KANISA KUMHUSU BIKIRA MARIA

Kanisa Katoliki linatafakari kuhusu mafumbo ya Umwilisho na Ukombozi wa Bikira Maria. Kanisa limetambua uwepo wa Maria na kushiriki kwake katika uwmwilisho na Ukombozi. Kanisa linamwelewa Bikira Maria kuwa, “**Mama wa Mungu**” (*Theotokos*), kama kweli Bikira, “**Mkingiwa dhambi ya Asili**” na “**mpalizwa mbinguni-roho na mwili”.**

**Mama wa Mungu *[Theotokos]***

- Katika mapokea na imani ambayo Kanisa linaungama, Bikira Maria ni kuwa kweli ni Mama wa Mungu. Maria ni mama wa Yesu Kristu ambaye ni Mungu kweli na Mwanadamu kweli. Kwa hiyo ni Mama wa Mungu. Hili ni fundisho la imani lililokubaliwa tangu zamani katika *Mtaguso wa Epheso 431*.
- Mababa Watakatifu walimwita Bikira Mtakatifu "**Mama wa Mungu**"(*Theotokos)*. Hii haimanishi kuwa asili ya Neno au umungu wake ulianzia kwake Bikira Maria, lakini mwili mtakatifu ambao ulitiwa uzima na roho, ambayo ni "Muungano wa asili mbili, ya **kimungu** na ya **kibinadam**u, katika nafsi moja=Kristo Mungu-Mtu (*Hypostasis*), alizaliwa naye.
- Fundisho hili lina msingi katika maandiko matakatifu [*Gal 4:4; Lk 1:32, 35,Lk 1:43,45,46; 20:31*]. Ni ukweli kuwa Maria ni Mama wa Yesu, Mwana wa Mungu. Hivyo yeye ni "*Theotokos*". Katika kila tarehe ya kwanza ya mwaka, tunamkumbuka Maria Mama wa Mungu.

***Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya Asili***

- Katika barua ya Papa (*Inffabilis Deus tarehe* 8 Desemba 1854), Pius IX alitangaza kuwa Kuzaliwa Bikira Maria bila dhambi ni mafundisho ambayo ni nguzo ya imani. Dogma yenyewe ilisema hivi: "*Bikira Maria* Mtakatifu sana, *mwanzo wa kutungwa kwake, alipendelewa na neema ya Mwenyezi Mungu, Kuwa Mama wa Yesu* Kristu, *mwokozi wa wanadamu wote,alikingiwa doa la dhambi ya asili*".
- Heshima ya Maria ndiyo ilikuwa sababu ya kukingiwa dhambi ya asili. Japo katika maandiko Matakatifu hamna uwazi wa Bikira Maria kukingiwa dhambi ya asili lakini kuna tafakari ya kina kutoka [*Mwa 3:15* "Mwanamke", *Lk 1:28*] "*umejaa neema*", [*LK 1:28]* "*Umebarikiwa kuliko wanawake wote*". Huu ni udhihirsho kuwa Maria ni Mtakatifu, pia huru kutoka dhambi ya asili.
- Malaika alimsalimia, "*umejaa neema*" na tena, "*usiogope, Maria kwa kuwa umepata neema za Mungu*", [Lk 1:28-30], hii pia linatupa mwelekeo wa kuelewa Maria alikingiwa

dhambi ya asili. Kadiri ya Agano jipya, neema ni zawadi ya Mungu, kumtoa Mwanawe [*Rum 8:32*] ambayo ina zawadi zingine nyingi. Na si zawadi iliyojificha, bali inamuathiri yule anayepokea na upendo pamoja na ukarimu wa mtoaji. Na ndivyo tunafahamu kuwa Mwanamke, "*aliyejaa neema*", tunaongea juu yake kama yule ambaye Mungu yumo ndani yake.

- Maria anaeleweka kama mwanamke ambaye Mungu yumo ndani yake kwa nafasi ya kipekee na amejawa na uwepo wa Mungu. Hii inamfanya awe huru kutokana na dhambi na amejawa sifa ya mng'aro wa Mungu. Huduma ya Maria kwa Elizabeti na wimbo wake wa shukrani ni ishara ya hali ya ndani ya moyo wake.

***Kupalizwa Mbinguni Bikira Maria***

*Sherehe hii husherehekewa tarehe 15 Agosti.*

- Konstitusio ya Kitume (*Munificentissimus Deus) ya* Pius XII tarehe 1 Novemba 1950, ilitangaza kupalizwa Mbinguni Bikira Maria kuwa ni fundisho la Imani (*dogma*). Ilitangazwa hivi, "*tunatamka, na tunatangaza kuwa imefunuliwa kwetu, kuwa Mama wa Mungu, kweli Bikira Maria baada ya kumaliza maisha yake hapa ulimwenguni alipalizwa mbinguni mwili na roho*". Maria ameingia utukufu wa mbinguni, ameshirikishwa utukufu wa Mwanawe.
- *Theolojia ya kupalizwa Maria Mbinguni*: Kupalizwa kwa mwili na roho ya Maria mbinguni ilikuwa ni zawadi kamili kutoka kwa Baba na si kitu alichofanikiwa mwenyewe. Utakatifu wa Kikristu, ukamilifu na Utakatifu wa Kanisa ni zawadi kamili kutoka kwa Mungu, na si matokeo ya kazi yetu. Hata hivyo mwelekeo wa mwanadamu ni kuingizwa katika maisha ya Utatu Mtakatifu. Jinsi ya Maria, kile kinachofanya Kanisa na kila Mkristu, ni neema: " *kwa neema umeokolewa katika imani; na hili si tendo lako, ni zawadi ya Mungu*"[*Eph 2:8*]. Neema ni swala la kwanza la Ukristo na sababu ya msingi wa Utakatifu.

- Kupalizwa Mbinguni Bikira Maria, ni ishara ya kuonyesha mwelekeo wa wanadamu wote. Mungu aliye Mtakatifu sana ataka tuishi naye milele. Kupalizwa Mbinguni Bikira Maria ni tumaini kwa wanadamu wote, kuwa huko ndiko tunaelekea. Hivyo basi mioyo yetu, mawazo na matendo ni lazima yawe na msingi wa uzima wa milele.

***Ubikiria wa Maria***

- Ni fundisho la Imani kuwa Yesu Kristu alizaliwa na Bikira Maria. Hivi ni kusema kuwa Maria ndiye alikuwa mzazi wa kibayologia pekee yake. Mwana wa Mtu hakuwa na baba wa kibayolojia; alitungwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Katika Mtaguso wa kwanza wa Konstantinopoli 381 uliongeza kwenye Kanuni ya Imani ya Nikea maneno haya: "*Kwa Roho Mtakatifu na Bikira Maria*" kurejea umwilisho wa Kristu.

## MAJINA YA MARIA

Bikira Maria amepewa majina kulingani na nyakati, mazingiria na matukio mbalimbali ambayo anawafikia watu kuwaletea ujumbe wa Mungu. Tutatakafakri juu ya baadhi ya majina Bikira Maria anapewa. Japo kuna majina hayo, Bikira Maria ni Yule Yule Mama wa Mkombozi. Katekisimu yatufundisha kuwa Mungu humwita kila mtu kwa jina. Jina la kila mtu ni takatifu. Na jina ni sanamu ya mtu. Linadai heshima kama ishara ya hadhi ya yule anayelichukua. Hivyo basi majina hayo yote Bikira Maria amepewa ni matakatifu na yanatuletea baraka za Mungu.

***Aliyejaa neema***

Sala ya Salamu Maria, yatuonyesha wazi kuwa Mungu amemjalia Maria neema. Maria amejaa neema kwa sababu Bwana yu pamoja naye. Na neema hii ni kuwa amejazwa uwepo wa Yule aliye chemichemi ya kila neema:

- Maria ambaye ndani yake Bwana Mwenyewe anakuja kukaa, anakuwa sanduku la agano, mahali ambapo utukufu wa

Bwana unakaa, yeye ni "*maskani ya Mungu pamoja na wanadamu*".

- Katika neema, Maria ametolewa wote kabisa kwa Yule anayekuja kukaa ndani yake na ambaye yeye atamtoa kwa ulimwengu.
- Salamu ya Malaika Gabrieli inadhihirisha kuwa Maria amebarikiwa kuliko wanawake wote na Yesu mzao wa tumbo lake amebarikiwa. Maria amebarikiwa kuliko vizazi vyote kwa sababu alisadiki katika utimilifu wa Neno la Bwana.
- Maria kwa imani yake ni Mama wa waamini, kwa njia yake mataifa yote ya dunia yanampokea Yule ambaye ni baraka yenyewe ya Mungu:-"*Yesu, mzao wa tumbo lako amebarikiwa*". Maria ametupatia Yesu Mwanawe.
- Maria ni Mama wa Mungu na Mama yetu. Tumkabidhi mahangaiko yetu na maombi yetu: anasali kwa ajili yetu kama alivyosali kwa ajili yake mwenyewe,"na *iwe kwangu kama ulivyosema*." Tunapojiaminisha kwa sala zake, tunajiachilia sisi wenyewe kwa mapenzi ya Mungu pamoja naye: "*mapenzi yako yafanyike*".
- "*Utuombee sisi wakosefu sasa na saa ya kufa kwetu*": Tunapomwita Maria atuombee tunakiri kwamba: tu wakosefu, maskini na tunajielekeza kwa "**Mama wa Huruma**" ambaye ni Mtakatifu sana. Tunajitoa kwake sasa katika "leo" ya maisha yetu. Na tumaini letu linapanuka kumkabidhi yeye tangu '*saa ya kufa kwetu'*. Awepo pale kama alivyokuwa katika kifo cha Mwana wake Msalabani. Saa ya kufa kwetu atupokee kama Mama yetu, ili atuingize paradiso kwa Mwanae, Yesu.
- Maria ndiye mkamilifu anayesali- sura ya Kanisa. Tunamwomba, tunaungana naye katika mpango wa Baba anayempeleka Mwanae kuwaokoa watu wote. Kama mwanafunzi aliyependwa, nasi tunampokea kwetu, Mama wa Yesu ambaye amekuwa Mama wa wote walio hai. Tunaweza kusali pamoja naye na kumwomba. Sala ya Kanisa

yategemezwa na sala ya Maria nayo imeunganika na Maria katika tumaini.

### *Aliyekingiwa dhambi ya asili*

Bikira Maria ana neema ya Mungu kwa ajili ya kumpokea Mwana wa Mungu hivyo basi:

- Malaika Gabrieli wakati wa kupasha habari alimsalimu kama "*uliyejaa neema*". Karne kwa karne Kanisa limetambua kwamba Maria alijazwa neema na Mungu. Alikombolewa tangu mwanzo wa kuchukuliwa kwake mimba. Ndicho kinatufundisha mafundisho ya imani juu ya kukingiwa dhambi ya asili yaliyotangazwa na papa Pio IX, mwaka 1854:
- Mwenye heri kabisa Bikira Maria, tangu nukta ya kutungwa kwake mimba, kwa neema na upendeleo wa pekee wa Mungu Mwenyezi, kwa kutazamia mastahili ya Yesu Kristo, Mwokozi wa wanadamu wote, alikingiwa na kila doa la dhambi asili. Kwa neema ya Mungu Maria amebaki safi kabisa na hakutenda dhambi yoyote maisha yake yote.

### *Daima Bikira*

Matendo makuu ya Mungu ni ya daima.

- Kuingia ndani ya imani juu ya umama na ubikira wa Maria, umeliongoza Kanisa kuungama ubikira wa kweli na wa daima wa Maria, hata katika kuzaliwa kwa Mwana wa Mungu aliyefanyika mtu. Kuzaliwa kwa Kristo, kwa uhakika "*hakukupunguza ukamilifu wa ubikira wake, bali kumeutakatifuza*".
- Liturjia ya Kanisa inamtukuza Maria kama = "*Bikira Daima*". Yesu ni Mwana wa pekee wa Maria. Lakini umama wa kiroho wa Maria unaenea kwa watu wote ambao Yesu amekuja kuwaokoa: "*Alimzaa Mwana ambaye Mungu alimweka, mzaliwa wa kwanza kati ya ndugu wengi*" yaani waamini. Maria anashiriki kwa mapendo ya kimama wakati wa kuzaliwa kwao na kuelewa kwao.

### *Eva Mpya*

- Katika Injili Maria anatambulika kama mwanamke aliyetangazwa, "**Maria mama wa Kristo**", kama "**Eva Mpya**" . Maria alikuwa wa kwanza kati ya wote na kwa namna ya pekee kufaidi ushindi ulioletwa na Kristo juu ya dhambi: alikingiwa na kila doa la dhambi ya asili, na katika maisha yake yote ya hapa duniani, kwa neema ya pekee ya Mungu, hakutenda dhambi yoyote.

### *Kiti cha Hekima*

- Maria, Mtakatifu kabisa, Mama wa Mungu, Bikira daima ni kilele cha utume wa Mwana na Roho Mtakatifu katika utimilifu wa nyakati. Kwa mara ya kwanza katika mpango wa wokovu na kwa sababu Roho wake amemtayarisha, Baba anapata "*makao*" ambamo Mwana wake na Roho wake wanaweza kukaa kati ya watu.
- Mapokeo ya Kanisa yamesoma mara nyingi, kuhusiana na Maria, mambo yaliyo bora sana juu ya hekima. Maria anaimbwa na kuwasilishwa katika Litrujia kama "**kiti cha Hekima**". Ndani yake, maajabu ya Mungu ambayo Roho atayatimiza katika Kristo na katika Kanisa yanaanza kujionyesha.

### *Mama wa Kanisa*

- Bikira Maria anatambuliwa na kuheshimiwa kama "*Mama kweli wa Mungu, na wa Mkombozi Yeye ni pia* " Mama kweli wa viungo vya Kristo, kwa sababu alishiriki kwa mapendo yake kuzaliwa kwa waamini ndani ya Kanisa, ambao ni viungo vya kichwa hicho.
- Katika Kanisa kazi ya Bikira Maria haitengani na umoja wake na Kristo, bali inatoka moja kwa moja humo.  Umoja huo unaonekana tangu kutunga mimba Kristo mpaka kifo chake. Baada ya Mwanawe kupaa mbinguni.

- Maria "*kwa sala zake alisaidia kuzaliwa kwa Kanisa*." Akiunganika na mitume na wanawake kadhaa, hata Maria aliomba kwa sala zake paji la Roho, ambaye wakati wa kutangazwa kuzaliwa kwa Bwana, yeye mwenyewe alishampata chini ya kivuli chake.
- Bikira Maria alitukuzwa na Bwana kama Malkia wa ulimwengu, kwa sababu alikuwa amefana sana na Mwanawe, Bwana wa mabwana, na mshindi wa dhambi na mauti. Kupalizwa kwa Bikira Mtakatifu ni ushirika kwa namna ya pekee ufufuko wa Mwanawe na ni utangulizi wa ufufuko wa Wakristo wengine. Kwa kuambatana kwake kabisa na mapenzi ya Baba , na kazi ya ukombozi ya Mwanawe, na Msukumo wote wa Roho Mtakatifu Bikira Maria ni mfano wa imani na wa mapendo kwa ajili ya Kanisa. Kwa sababu hiyo yeye, "*kwa hakika ni Mwanakanisa kabisa*, *"yeye ni*, "*mfano Mtimilifu*" wa Kanisa.

### ***Mama wa Mungu***

- Maria ni kweli Mama wa Mungu kwa kuchukua mimba ya kibinadamu ya Mwana wa Mungu katika tumbo lake: " Ni Mama wa Mungu siyo kwa sababu Neno wa Mungu ametwaa kwake asili yake kimungu, lakini kwa sababu ametwa kwake mwili mtakatifu wenye roho yenye akili, akafanana nao katika nafsi yake, na ndivyo tunakiri kuwa Neno amezaliwa kadiri ya mwili.
- Maria ni kweli , " *Mama wa Mungu*", kwa sababu ni Mama wa Mwana wa milele wa Mungu aliyefanyika Mtu, ambaye Yeye mwenyewe ni Mungu.

### ***Mama wa walio hai***

- Bikira Maria "*alishiriki wokovu wa binadamu kwa imani yake na utii wake wa hiari. Alitamka ndiyo yake* "kwa niaba ya binadamu wote". Kwa utii wake amekuwa Eva mpya, mama wa Walio hai.

### *Mama wa Yesu*

- Mjakazi wa Bwana Maria amebaki '*bikira*' katika kutunga mimba ya Mwanawe, bikira katika kumzaa; bikira alipomchukua, bikira alipomlisha kifuani pake, bikira daima. Kwa uwepo wake wote alikuwa ni mjakazi wa Bwana [*Lk 1:38*]. Baadhi ya majina mengine ni haya:-Mpalizwa Mbinguni, Mtetezi, Msaidizi, Mfadhili.

## IBAADA KWA BIKIRA MARIA

Bikira Maria mwenyewe aliimba kuwa "*vizazi vyote wataniita mbarikiwa*" , baada ya kumtembelea Elizabeti aliyetambua kuwa ni mama wa Mwokozi. Uchaji wa Kanisa kwa Bikira Maria ni wa ndani kabisa katika ibada ya Kikristo. Bikira Mtakatifu, "anaheshimiwa kwa haki na Kanisa kwa ibaada ya pekee. Kwa kweli tangu nyakati za kale zaidi, Bikira Mwenye heri ameheshimiwa kwa cheo cha "*Mam*a *wa Mungu*", waamini wanamkimbilia ulinzi wake, wanamwita katika hatari zao zote na mahitaji yao.

Ibada hiyo, ingawa ni ya pekee kabisa ni tofauti kimsingi na ibada ya kuabudu inayotolewa kwa Neno aliyemwilishwa, pia kwa Baba na kwa Roho Mtakatifu; ile ya kwanza inakuza ya pili. Ibada kwa Bikira Maria huonekana katika sikukuu za Kiliturjia alizowekewa Mama wa Mungu: na katika sala za Maria, kama Rosari takatifu, "*Muhtasari wa Injili yote*".

Katika kuadhimisha kila mwaka mafumbo haya ya Kristo, Kanisa humheshimu kwa upendo wa pekee Maria mwenye heri, Mama wa Mungu, ambaye ameunganika na Mwana wake kwa namna isiyoweza kutengwa katika kazi ya ukombozi. Tena ndani ya Maria, Kanisa huheshimu na kutukuza tunda bora kuliko yote ya ukombozi, na hutafakari kwa furaha, kama katika mfano usio na doa wa yale yote linayoyatamani na kuyatumaini kwa ajili yake.

### Sala ya Rozari

Rozari takatifu ni sala ambayo inapendwa sana na inachukua nafasi muhimu sana kiundani kwa ajili ya sala ya Kikristo.

Mamlaka fundishi ya Kanisa na pia imedhibitishwa na watakatifu kuwa; sala hii ya rozari inaendana na mafundisho ya mtaguso wa pili wa Vatikano. Inaelezea nafasi ya Bikira Maria, ili waamini wote waweze kumjongea mwombezi na mwokozi. Bikira Maria anawaunganisha waamini na Kristo.

Ni kweli kuwa katika sala ya rozari, Bikira Maria awafundisha watoto wake jinsi ya kuungana na fumbo la Kristo. Hata hivyo Kanisa linatilia uzito kwa ibaada za Bikira Maria kwa wote waliopokea wito wa kumfuata Kristo. Mtakatifu Yohane Bosko alipendekeza kwa wafuasi wake, hadi kuwaeleza kuwa shirika lake msingi wake umetokana na Bikira Maria.

Papa Paulo VI katika barua yake "*Marialis cultus*", alitoa fundisho kuu kuhusu sala ya rozari, akichukulia ule umuhimu wa ndani na kupendekeza kwa waamini kufanya ibaada. Alisema rozari ni:

- *Ni asili ya kuinjilisha*: Mafungo yote ya rozari yanatokana na Injili, tunaweza kusema ni mkusanyiko wa Injili yote.
- *Inabeba mafundisho ya Kristo*: - Rozari inaonyesha mafumbo yote ya ukombozi.
- *Inahusika katika liturjia*: Rozari inachukua asili yake kutoka liturjia na kuelekeza waamini kwenye liturjia. rozari na liturjia ina mwelekeo mmoja tu, mwelekeo wa ukombozi wa Kristo.

Katika kusali rozari, jambo la muhimu ni kutafakari juu ya yale mafungo ambayo yanamwelekeza mtu katika wazo la kiroho. Kusali kwa rozari kwa hitaji utulivu, umakini ambao unamwelekeza anayesali katika kutafakari mafumbo ya maisha ya Bwana ambayo yako wazi katika macho ya Bikira Maria aliyempokea kwanza.

Rozari hufananishwa na shule ya ibada ya ndani sana. Rozari hulinda na hufundisha waamini kwa malezi bora ya kiroho.

## MARIA MSAADA WA WAKRISTO

**Kanisa la Maria Msaada wa Wakristo huko Torino**

Maria Msaada wa Wakristo



Maria Msaada wa Wakristo ni jina la heshima kwa Mama Bikira Maria. Ibaada ya Bikira Maria ni tendo kamili katika Kanisa Katoliki ambapo Sikukuu yake husherehekewa tarehe 24 Mei kila Mwaka. Mtakatifu **Yohane Chrsysostom** ndiye wa kwanza kutumia sifa **–"Maria Msaada wa Wakristo"** mwaka 345. **Mt. Yohane Bosco** aliendeleza ibada ya Maria katika kazi zake. Sifa "*Maria Msaada wa Wakristo*", huhusishwa na Msaada wa Mungu ambao Wakristo walipata katika Europa [ *Latin na Greek*], Afrika Kaskazini, na nchi kama Syria, uturuki  na Uarabuni.

Wakristo walipewa Msaada na Mama Bikira Maria dhidi ya makundi ya Kiislamu ambayo yaliwashambulia Wakristo na kuwalazimu kuwacha dini yao na kufuata Uislamu. Baba Mtakaktifu **Pius V** aliita majeshi ya Wakristo kuilinda Europa na

aliwauliza waamini kusali rozari kwa Mama Bikira Maria. Kwa sala ya rozari waislamu walishindwa katika vita vyote. Ushindi huo wa Kanisa unaaminiwa kuletwa na Mama Bikira Maria. Na ndivyo jina "*Maria Msaada wa Wakristo*" lilienea; kwa sababu waliamini kuwa ushindi wao ulitokana na mama wa Mwokozi.

### Sikukuu ya Maria Msaada wa Wakristo

Zamani Bikira Maria alipewa sifa zifuatazo: Mama wa Mungu, Maria Msaada wa Wakristo. Baba Mtakatifu Pius V aliweka sifa hii katika Litania ya Loreto baada ya vita vya Lepanto. Sikukuu ya Maria Msaada wa Wakristo ilitangazwa rasmi na **Papa Pius VII**. Mfalme Napoleon I alimweka mateka Papa huyo mnamo tarehe 5 Juni, 1808. Aliwekwa huru tarehe 17 Machi 1814 Jioni ya sikukuu ya Maria Mama wa huruma.

Papa Pius VII aliona kuwa ushindi uliopatikana kwa Wakristo ulitokana na Msaada ulioletwa na Mama Bikira Mari; nyakati za vita dhidi ya Wakristo; Papa aliwahimiza Wakristo wasali rozari na majitoleo mengine. Wale walioenda vita walipata nguvu za kushinda. Kwa namna hiyo Mama Bikira Maria alionekana wazi kuwa msaada wa Wakristo. Baada ya Papa kutoka uhamishoni, alienda kusali kwenye makanisa ya Bikira Maria akitoa shukrani. Huyu Baba Mtakatifu alirudi Roma 24 Mei 1814. Kuonyesha moyo wa shukrani kwa Bikira Maria Mtakatifu; Baba Mtakatifu Pius VII, tarehe 15 Septemba 1815, aliweka sikukuu ya Maria Msaada wa Wakristo iwe kila mwaka tarehe 24 Mei. Sikukuu hii ilianza kusherehekewa tarehe 24 Mei 1913.

### Walioeneza ibada ya Maria Msaada wa Wakristo

Mtakatifu Yohane Bosko na Mt. Vincent Pallotti walieneza ibada kwa kwa Maria Msaada wa Wakristo huko Italia na mahali kwingi. Mwaka 1868 Yohane Bosko alijenga Kanisa kuu la Maria Msaada wa Wakristo kule Torino -Italia na akaanzisha shirika la, "*Mabinti wa Maria Msaada wa Wakristo*" (*The Daughters of Mary Help of Christians*). Kulingana na sifa hii aliyopewa Bikira Maria; Kanisa katika utamaduni wake limesisitiza mambo mawili:

❖ *Katika sikukuu ya Maria Msaada wa Wakristo; Kanisa linatilia mkazo wa wito wa Bikira Maria kuwa mwombezi na msaidizi katika kuvipiga vita dhidi ya dhambi katika maisha ya mwaamini (Mkristo).*

❖ *Kanisa linamwangalia Bikira Maria kuwa yule ambaye anawasaidia Jumuiya ya Wakristo kwa maombezi yake, kulilinda Kanisa dhidi ya wale wapinga Kristo na vikwazo mbalimbali.*

Baada ya Mtaguso wa Vatikano II; Sikukuu hii ilifikiriwa kuadhimishwa Jumapili kabla ya tarehe 24 Mei au Jumapili inayofuata. Sikukuu hii ya Maria Msaada wa Wakristo ni muhimu sana, Mtakatifu Yohane Bosko mwanzilishi wa shirika la Waselesiani wa Don Bosko( **Salesians of Don Bosco**), kazi zake zote aliziweka chini ya ulinzi wa Maria Msaada wa Wakristo, kuanzia Kanisa Mama la huko Torino 9 Juni 1868. Waselesiani wameeneza ibaada hii mahali popote walipoenda ambapo wanaendesha Utume.

**Ekaristi Takatifu na Upendo kwa Bikira Maria**

Nyakati nyingi Wakristo ulimwenguni wamepata miujiza ya Maria Msaada wa Wakristo. Mojawapo ni ule ushindi wa Lepanto, wakati kundi la Waislamu, wazushi na watu wasio dini walianza kushambulia Ulaya. Baba Mtakatifu Pius V aliwasihi Wakristu waanzishe vita vya kiroho kwa kusali rozali na maandamano ya Ekaristi Takatifu kila mahali. Ni kwa nguvu za Ekaristi Takatifu na sala ya rozari vita hivyo vilishindwa.

Wakristo katika makundi makubwa walisali rozari hadharani *katika* maandano mbalimbali. Mwanzoni mwa vita Wakristo walishindwa sana, lakini baadaye walianza kupata ushindi. Ushindi wa vita hivyo ulileta wazi na ibada kwa Ekaristi Takatifu na sala ya rozari. Kwa heshima ya utukufu wa Mungu na ushindi kwa njia ya ya Ekaristi Takatifu na sala ya rozari; Baba Mtakatifu Pius V aliamuru sikukuu ya rozari Takatifu na akaaongeza sala, "*Maria Msaada wa Wakristo, Utuombee*".

Mwaka 1809, sala na maombezi pia zilimfikia Maria Msaada wa Wakristo. Mfalme Napoleon wakati alitengwa na Kanisa aliamua

kumteua Baba Mtakatifu Pius, VII. Alimkandamiza aweke mkataba kuwa mfalme ndiye atakuwa na uamuzi wa mwisho katika maswala ya Kanisa na jamii huko Ufaransa. Ni kwa mujibu wa ibada kwa Ekaristi Takatifu na sala ya rozari Baba Mtakatifu Pius VII aliwekwa huru. Tarehe 24 Mei 1815, Baba Mtakatifu aliweka wakfu siku hiyo kwa heshima ya Bikira Maria na akaanzisha siku kuu ya Maria Msaada wa Wakaristo.

**Maria Msaada wa Wakristo na Yohane Bosko**

Roho wa Mungu aliamsha ndani ya Mtakatifu Yohane Bosko, ibada kwa Maria Msaada wa Wakristo (1815-1888) kwa ajili ya wokovu wa vijana. Katika miaka yake ya upadre Yohane Bosko alieneza ibaada ya Moyo Mtakatifu wa Maria na Mama wa Huruma katika jina la Maria Msaada wa Wakristo. Mwaka 1863, Yohane Bosko alianza kumheshimu Bikira Maria katika sifa ya "*Maria Msaada wa Wakristo*".

Wapinzani wa Kanisa walikuwa wameanza kumshambulia Baba Mtakatifu na Kanisa. Mwaka 1862, picha ya Bikira Maria iliyochorwa ikampendeza Askofu mkuu wa *Spoletto* ambaye aliiheshimu kwa sifa "**Maria Msaada wa Wakristo**". Yohane Bosko aliongozwa na Roho wa Mungu ajenge Kanisa ambalo litakuwa chini ya ulinzi wa Maria Msaada wa Wakristo huko Torino - Italia.

Hata hivyo Yohane Bosko alipata vikwazo vingi sana kutoka kwa viongozi wa serikali, wapinga Kanisa na pia alikosa uwezo wa kifedha. Basilika ya Maria Msaada wa Wakristo ilimalizika kimujiza mwaka 1868. Kwa Yohane Bosko, msaada wa Maria ulikuwa muhimu sana sababu kulikuwa na Wakristo ambao hawakuwa wenye bidii katika imani, wadhambi na watu wema. Kanisa Katoliki pia lilikuwa katika mashambulizi. Kwa kumwita Maria Msaada wa Wakristo, alimwezesha kufanya miujiza na kufanya bidii kuwaongoa vijana walio kuwa wengi. Alifanya bidii sana kueneza ibada kwa Maria Msaada wa Wakristo, aliwasihi watu kuwa na imani kwa maombezi ya Bikira Maria. Mara nyingi alisema, "uwe *na ibada kwa Bikira Maria, utaona miujiza*"

## KANISA LA MARIA MSAADA WA WAKRISTO HAPA KENYA



Waselesiani wa Don Bosko kutoka India walifika hapa Kenya mwaka wa 1982, walifikia Korr kwanza hapa Kenya na Tanzani baadaye Uganda na Sudan. Pia Waselesiani wa Don Bosko wamekuwepo katika nchi zingine za Afrika tangu hapo zamani. Waselesiani hao waliotoka India, walianzisha ibada ya Maria Msaada wa Wakristo na karama ya Mtakatifu Yohane Bosko mahali popote walipoenda. Mwaka 1992 Kanisa la Maria Msaada wa Wakristo lilifunguliwa hapa mji mkuu wa Kenya - Nairobi sehemu ya Upperhill. Hapo ndipo palipo makao makuu ya Waselesiani wa Don Bosko hapa Afrika Mashariki. Kanisa hilo lilifunguliwa rasmi na Mkuu wa Shirika la Waselesiani Egidio vigano mwaka 1993. Ni sehemu takatifu kwa Waselesiani wa Don Bosko. Mnamo mwaka 2011, masalia ya Mt. Yohane Bosko yalipitishwa katika vituo vyote vya Mtakatifu Yohane Bosko ulimwenguni mwote, ilikuwa namna ya kujiandaa kwa Yubilee ya miaka mia mbili tangu kuzaliwa Mt. Yohane Bosko. Safari hii

ilileta baraka hapa Afrika mashariki, miujiza mingi ilitendeka. Zilikuwa siku za sala maalum kwa ajili ya kumshukuru Mungu.
Hapa Kenya tuna baraka za pekee na neema za Mungu. Mkuu wa Shirika la Waselesiani na Kamati yake walitoa masalai ya Mt. Yohane Bosko kwa hapa Kenya kwa ajili ya Afrika nzima. Tarehe 28 Januari 2017, Masalia ya Mtakatifu Yohane Bosko, yalihamishwa kutoka seminari kuu ya Don Bosco Utume hadi katika Kanisa la Maria Msaada wa Wa Wakristo Nairobi Upperhill. Ilikuwa ni siku kubwa mno, iliyo ambatana na sala ya Misa Takatifu. Vijana kwa watoto, watu wazima wote walifika kwa wingi toka pande zote za vituo vya Mt. Yohane Bosko. Masalia hayo yaliwekwa chumba maalum ndani ya Kanisa kuu.
Don Bosko Upperhill kwetu Waselesiani ni sehemu takatifu ya hija. Kanisa la Maria Msaada wa Wakristo ni ishara ya upendo kwa Bikira Maria. Masalia ya Mt. Yohane Bosko ni ishara ya uwepo wake kati yetu. Na anaendelea kuziongoza kazi alizopewa na Mungu ndani ya Waselesiani wa Don Bosko. Don Bosco Upperhill ni sehemu takatifu ya hija kwa Waselesiani na pia kwa watu wote. Masalia haya ya Mt. Yohane Bosko yamepeanwa kwa ajili ya Afrika yote. Ni bahati ilioje na neema za Mwenyezi Mungu.
Kanisa hili la Maria Msaada wa Wakristo katika atare kuu nyuma yake, utapata picha iliyounganishwa vizuri ya njozi ya Don Bosko akiwa miaka tisa. Ni picha inayovutia sana, na pia kutukumbusha wito wa Mungu kwa mwanzo wa Shirika la Waselesiani wa Don Bosko. Katika hiyo picha, kuna Yesu, Maria mama yake, vijana, wanyama na Yohane Bosko. Kwa picha maelezo yote ya njozi yake yanaonekana wazi. Katika kikanisa kilicho chini kabisa, pia kuna picha nyingi za Don Bosko zilizochworwa na msani D’sasi. Kuna picha ya mji wa Nairobi, vijana, Mabinti wa Maria Msaada wa Wakristo, Mtakatifu Yohane Bosko. Kila siku kuna misa katika Kanisa hili ndogo. Waamini wanapata nafasi ya misa asubuhi, saa saba mchana na jioni. Kweli ni mahali patakatifu pa kumsifu Mungu. Hapa chini ni picha za Kanisa Kuu la Maria Msaada wa Wakristo.

## KANUNI ZA USHIRIKA WA MARIA MSAADA WA WAKRISTO

***UTANGULIZI NA KIAMBATANISHO CHA KANUNI***



**Mafundisho Mafupi ya Maria**

Picha hii ilikuwa ni wazo fupi la Don Bosko; alimwomba msani Tommaso Lorenzone kuichora mnamo1865, na baada ya miaka mitatu ya kazi, picha hiyo kubwa iliwekwa mahali ilipo katika Basilika. Don Bosko alieleza kwa maneno haya:

“Bikira Mtakatifu anaelea katika bahari ya mwanga na ukuu amezungukwa na jeshi la malaika, ambao wanamweshimu kama Malkia wao. Kulia ameshika fimbo, alama ya nguvu; na kushoto anamshikilia Mtoto, ambaye amefumbua mikono, anatolea kwa namna hii neema na huruma kwa wote ambao wanamkimbilia Mama yake mpendwa. Kila pande na chini ni Watakatifu Mitume na Wainjilisti. Wamejawa na furaha, kama kusema “*Malkia wa Mitume, Utuombee*”, wanamwangalia Bikira Mtakatifu kwa mshangao.

Katika msingi wa picha ni mji wa Torino, na Madhabahu ya *Valdocco* inayoonekana na *Supergo* kwa umbali.

Maelezo ya Don Bosko, yanamaanisha kuwa picha hiyo ni halisi inayoonyesha heshima,

“**Maria, Mama wa Kanisa**”.

Maria , kwa sababu, ni Mama wa Mwana wa Mungu, Yeye ni Malkia wa mbingu na nchi; Kanisa lote, likiwakilishwa na Mitume na Wataakatifu, linamtangaza kama Mama na Msaidizi mwenye Nguvu.

## KANUNI MPYA ZA MARIA MSAADA WA WAKRISTO Julai 2003

**DIREZIONE GENERALE OPERE DON BOSCO**
**Via della Pisana, 1111 – 00163**
**Roma Gombera Mkuu**

**Utambulisho wa Kanuni mpya kwa wanachama wa ushirika.**

Kwa Wanachama,

Katika Sikukuu ya Mt. Yohane Bosko, baba na mwansilishi wetu, ninafuraha kutambulisha kanuni hii mpya kwenu. Haya ni matokeo ya kazi ya ziada kwa sehemu ya kila mmoja na vikundi – na sana kwa namna ya pekee kwa kikundi cha Kwanza huko Torino – kwa nyote nawashukuru. Kanuni hizi zimeidhinishwa na

kitengo cha mashirika ya maisha ya wakfu na jumuiya za maisha ya utume, tarehe 7 Oktoba 2003.

Kwa kuwa Kanuni hizo zimesharudiwa na kurekebisha, ni ishara kuwa ushirika huu upo hai, ambao una nia ya kuendelea katika kazi ya utume na kiroho katika uhusiano mwema na Kanisa pamoja na Familia ya Waselesiani. Ni pia ishara kweli ya kilelezo cha uwajibikaji wa nguvu na uaminifu kwa Don Bosko, ambaye alitaka ushirika wa Maria Msaada wa Wakristo kuwa alama ya shukrani kwa uwepo wa kimama wa Bikira Maria katika maisha yake na kazi zake, na mfano wa maisha ya Kikristo ambao kiini chake ni elimu, upendo na kumuenzi Bikira Maria.

Nimetumaini yangu ya dhati kuwa wanachama wote wa ushirika huu, wataweza kusoma kwa undani maandishi haya mapya na kupata roho ya Waselesiani iliyoelezwa ndani yake. Ninawakabidhi nyote kwa Mama yetu, Msaada wa Wakristo.

**Roma, 31 Januari 2004**
**Sikukuu ya Mt. Yohane Bosko**
**Fr Pascual Chávez V.**
**Mkuu wa Shirika**

**AMRI**

Ushirika wa Maria Msaada wa Wakristo, ulianzishwa na Mt. Yohane Bosko, "kuendeleza heshima kwa Sakramenti Takatifu na upendo kwa Maria Msaada wa Wakristo", kisheria ilisimikwa katika madhabahu ya Maria Msaada wa Wakristo huko Torino tarehe 18 Aprili 1869, na kuinuliwa na Mwenyeheri Pius IX tarehe 5 Aprili 1870 katika daraja la jumuya kubwa, ambayo ni mali ya Familia ya Waselesiani.

Msaidizi wa Mkuu wa Shirika (*The Vicar of the Rector Major*) ametambulisha kanuni hizi kwa ofisi kuu ya Utume kwa ajili ya kibali.

Kitengo cha mashirika ya maisha ya wakfu na jumuiya ya maisha ya Utume, baada ya kutathimini kwa uangalifu, Kanuni zilizotajwa, liliidhinisha katika lugha ya Kitaliano iliyowekwa katika hifadhi, masharti yote ya sheria yalifuatwa.

Kitu chochote kinyume hakikubaliki.

**Ilitolewa Vatikani, 7 Oktoba 2003,**
**Sikukuu ya Bikira wa Rozari.**
**Eduardo Card. Martinez Somal**
**Mkaguzi**
**Piergiorgio Silvano Nesti,**
**C.P. Katibu**

## KANUNI ZA JAMII YA MARIA MSAADA WA WAKRISTO

Masahisho ya Julai 2003

DIBAJI

Akisukumwa na Roho Mtakatifu kwa ajili ya mahitaji ya dharura na ishara za nyakati, Don Bosko, alianzisha katika utume wake chama kikubwa cha watu ambao wangefanya kazi kwa namna mbalimbali kwa ajili ya faida ya vijana na kundi la wale wafanyikazi.Ushirika wa Maria Msaada wa Wakristo ulianzishwa na Don Bosko kama chombo maalum cha "*Kutangaza heshima kwa Sakramenti Takatifu na upendo kwa Maria Msaada wa Wakristo*".

Ilizinduliwa kisheria katika madhabahu ya Maria Msaada wa Wakristo huko Torino 18 Aprili 1868, na "*aliitazamia kuwa sehemu maalum katika jumuiya ya Waselesiani*" *(Fr Pietro Ricaldone, Maria Ausiliatrice, Colle Don Bosco 1951, p. 83).*

Katika mhutasari mfupi 5 Aprili 1870, Pius IX aliuinua katika darala la Jumuiya kubwa, na ibada ya pamoja ya vyama ambavyo vinaibuka katika sehemu mbalimbali za ulimwengu kwa kijana hilo na nia hiyo.

5 Julai 1989, Mkuu wa Waselesiani, Pd. Egidio Viganò pamoja na halmashauri yake, rasmi walitambua ushirika wa Maria Msaada wa Wakristo kama mwanachama wa familia ya Waselesiani.

TESTUS APPROBATUS

Romae, die 7-10-2003

## KANUNI YA USHIRIKA WA MARIA MSAADA WA WAKRISTO

### *ASILI NA SABABU YA USHIRIKA WA MARIA MSAADA WA WAKRISTO [ADMA]*

***Kipengee1***

*Tendo la Msingi*

Baada ya Don Bosko kujenga madhababu ya heshima ya Bikira Maria ambayo yaliwekwa wakfu kwa ajili ya Msaada wa Wakristo [Torino 1868], kwa kufuatia ishara zake alizopata kutoka njozi, alielewa baada ya mwaka ilikuwa hamu ya kujenga Basilika. Ushirika wa wafuasi wa Maria Msaada wa Wakristo(18 April 1869) una wajibu wa kueneza ulimwenguni mwoto ibada kwa Maria Maria kwa jina hilo.

Kanisa la Maria Msaada wa Wakristo, ndilo kiini cha kusambaza utume huu, ulimwenguni pote, mahali hapa kwa Don Bosko ilikuwa ukamilifu wa kazi zake zote, kisima cha neema na madhababu ya ulimwengu.

Upendo wa Don Bosko kwa Maria Msaada wa Wakristo unapatikana katika ushirika huu kwa namna ya maelezo ya kulinda na kutetea imani.

“Sisi Wakristo ni lazima tuunganike katika nyakati ngumu. Kuwa miongoni mwa wale wanaotenda wema, ni chemichemi inayochangamsha na kuchochea wema kwetu, bila kuelewa zaidi”[MB 7, 602)

Uzoefu, “unatuoenyesha kuwa utume wa Maria kama mama wa Kanisa na Msaada wa Wakristo, alioanza duniani, unaendelea kutoka mbinguni kwa namna ya ajabu kwa ulimwengu wote”.

(G.*BOSCO, Meraviglie della Madre di Dio invocata sotto il titolo di Maria Ausiliatrice, Torino, 1868, p. 45).*

Uwepo huu wa Kimama wa Bikira Maria ndio msingi wa Ushirika na msukumo wa majukumu ya wafuasi kwa ajili ya huduma ya Ufalme wa Mungu.

***Kipengee 2***

*Asili na Sababu*

Ushirika wa Maria Msaada wa Wakristo unatoa nafasi ya kukutana kwa waamini ambao hushiriki kazi maalumu ya Bikira Maria.

Katika Kanisa, Ushirika wa Maria Msaada wa Wakristo ni ushirika wa hadharahi wa waamini tukirejelea Sheira za Kanisa [Kan. 298-320]. Tena ushirika huu una sifa ya sheria za Kanisa.

Katika nchi zote ushirika huu waweza fuata usajili wa kisheria, hata hivyo ushirika huu si wa kisiasa, au wakutengeneza faida.

Ushiriki huu wa Maria Msaada wa wakristo unatoa mwongozo wa utakatifu kwa ajili ya utume wa Waselesiani[ ni mapenzi yake Bikira Maria tumheshimu kwa jina la Maria Msaada wa Wakristo. Nyakati zetu ni ngumu, twahitaji huyu Bikira Mtakatifu kutusaidia kutunza na kulinda imani ya Kikristo" MB 7,334]. Kwa njia ya pekee Don Bosko alianzisha ushirika huu ili kuwashirikisha wafanya kazi katika maisha ya kiroho na utume wa Shirika la Waselisiani, kama kikundi cha pili maalum katika kazi zake [GC 24, 80]

Ushirika huu, unatoa nafasi ya pekee kabisa kwa ajili ya Ibada kwa Ekaristi Takatifu na upendo kwa Maria Msaada wa Wakristo katika kila namna, kwa matumizi ya binafsi au kwa ibada hadharani ambayo imeidhinishwa na Kanisa.

Inatimiza wajibu wake kwa ushirika na utii kwa maaskofu wa Kanisa na ushirikiano na vyama vingine vya Kanisa, hasa Familia ya Waselesiani.

Jina lake rasmi ni Ushirika wa Maria Msaada wa Wakristo au ASSOCIATION OF MARY HELP OF CHRISTIANS (AMHC), na makao yake makuu yapo Torino, via Maria Ausiliatrice 32, karibu na madhababu ya Maria Msaada wa Wakristo.

***Kipengee 3***

*Ushirika huu katika familia ya Waselesiani*

Wafuasi wanaunda sehemu ya Familia ya Waselesiani, “kwa njia ya heshima kwa Msaada wa Wakristo kadiri Don Bosko alivyo weka msingi. Kuwa mfuasi ni kujitolea kumheshimu Maria, msaada na Mama wa Kanisa, kwa kushiriki utume wa Don Bosko kwa watu, hasa, vijana na zaidi katika kulinda na kuiteta imani ya Kikristo”.(*Egidio Viganò, Lettera Al Rettore del Santuario di Maria Ausiliatrice a Torino del 24/07/1989).*

Katika Familia ya Waselesiani, ushirika huu unahamasisha na kueneza ibada kwa Maria kama namna ya kuinjilisha na kuwasaidia watu, hasa vijana na wale maskini.

Ushirika huu unatambua [Rector Major] , mwandamizi wa Don Bosko, kama baba na umoja wa Familia ya Waselisiani wote.

***Kipengee 4***

*Wajibu wa kila mwanachama*

Ufuasi kamili kwa ushirika huu, yadhihirisha kufuata kuwajibika, hasa katika familia na mahali unaishi, na sehemu za kazi na wale wote unashirikiana nao.

Bidii na heshima ya kushiriki maisha ya Liturjia, kwa kuungana na Kanisa ambalo Maria ni sura na mfano ; na hasa kwa namna ya kipekee kwa Sakramenti ya Ekaristi na Sakramenti ya Kitubio, na jinsi ya kuishi binafsi maisha ya Ukristo:

- Kuishi na kueneza ibada kwa Maria Msaada wa Wakristo kadiri ya roho ya Don Bosko, hasa katika Famila ya Waselisiani(E*gidio VIGANÒ, Circular Letter: Mary renews Don Bosco’s Salesian Family in ASC 289 January*-*June 1978);*
- Kufanya upya, kuimarisha na kuishi ibada na maisha ya kiroho kwa pamoja:
- *Kumbukumbu ya Maria Msaada wa Wakristo kila Mwezi tarehe 24;*
- *Kusali rozari;*

*- Novena kwa maandalizi ya Sikukuku ya Maria Msaada wa Wakristo;*
*- Baraka ya Maria Msaada wa Wakristo;*
*-Hija kwa mahali patakatifu pa Maria;*
*- Maandamano ya sala;*
*- Kushiriki maisha ya parokia: Liturjia, Katekesi, kuwatembelea wagonjwa na wazee, na mahitaji na huduma zingine katika Kanisa.*
*-Kumuenzi Maria kwa namna ya kuishi maisha ya Ukristo katika familia yako na pia kuwa mkarimu na yule ambaye anakaribisha;*
*- Kujihusisha na sala pamoja na matendo mema dhidi ya vijana masikini na watu wengine wanaohitaji;*
*- Kusali na kuwaimarisha walei, watawa na wale amabo wana vyeo ndani ya Kanisa na kwa namna ya pekee Familia ya Waselisiani;*
*- Kila siku kuishi maisha ya kiroho yenye mwelekeo wa fadhila za Injili, hasa kumshukuru Mungu kwa maajabu yanaoyoonekana katika kazi zake, na kuwa mwaminifu kwake hata katika nyakati za mateso na msalaba, kwa kufuata mfano wa Maria.*

***Kipengee 5***

*Kuwa mkarimu kwa zawadi za kiroho*

Wafuasi hushirikishana faida ya neema na maisha ya kiroho ambayo kwayo ni rasmi kwa ushirika na kwa yale katika familia ya Waselesiani(*Wafuasi hushiriki katika msamaha na faida ya kiroho ambayo ni ya kipekee kwa chama na familia ya Waselesiani. Tumepewa katika Nyongeza II maelezo muhimu kwa ajili ya kutusaidia kuepuka matendo amabyo hayaendani na nia ya Kanisa*)

Zaidi, faidi ya maisha ya sala na ibada inayotolewa katika Basilika la Maria Msaada wa Wakristo huko Torino na katika makanisa mahali ushirika huu umeanzishwa.

Mfuasi akifa, wafuasi wengine katika kikundi wanaalikwa kushiriki katika Ekaristi ya walio katika mateso na huzuni.

## II. MUUNDO WA USHIRIKA WA MARIA MSAADA WA WAKRISTO

### *Kipengee 6.*

*Ushirika*

Katika mtindo wa Don Bosko, muundo upo kwa ajili ya huduma kwa kila mmoja na ni rahisi sana na yenye kuwezekana, na inaweza kutumika katika namna mbalimbali na kwa nchi mbalimbali.

Ni ukweli kuwa: ni jambo la muhimu kuwa kazi ya Don Bosko iliingiana na maisha ya kawaida hata katika mipangilio yake, ambayo yajieleza. Aliweza kuonyesha wazi majukumu ya kuendesha, kuimarisha na kukua"(*Viganò, Letter to the Rector of the Sanctuary of Mary Help of Christians in Turin, 24 July 1989).*

### *Kipengee 7.*

*Usimikaji wa ushirika mashinani*

Kwa njia ya [Kan. 312-317] na nafasi ya Shirika la Waselesiani, ni wajibu wa mkuu wa Waselisiani katika kanda kusimika Ushirika wa Maria Msaada wa Wakristo katika vyuo vya Waselesiani na Mabinti wa Maria Msaada wa Wakristo katika sehemu anayotawala. Kwa hali zingine barua ya Askofu wa mahalia inayoidhinisha huhitajika.

### *Kipengee 8.*

*Mkusanyiko*

Baada ya kusimikwa rasmi, maombi yatakiwa kutumwa haraka kwa ajili ya mkusanyiko. Yatumwe huko sehemu takatifu ya Maria Msaada wa Wakristo Torino- *Valdocco*, ili kumaliza uidhinishaji wa mkusanyiko kwa Ushirika wa Maria Msaada wa Wakristo.

Hati kamili, ambayo imetiwa sahihi na Mkurugenzi wa mahali patakatifu, ndiyo itakuwa hati rasmi ya uanachama. Inashauriwa

kuitunza katika hifadhi maalum na kivuli chake kubandikwa sehemu ambayo inaweza kuonekana kwa kila mtu.

***Kipengee 9***

*Ushirika na mahali patakatifu pa Maria Msaada WA Wakristo huko Torino*

"Ushirika wa Maria Msaada wa wakristo kwa namna ya pekee imeunganishwa na mahali patakatifu kule Torino – *Valdocco*. Inaweza kusemwa pia kwamba Maria hakuonekana wazi katika ujenzi wa wa mahali patakatifu, kwa maneno ya Don Bosko, lakini kuanzia pale alianza kuweka ulinzi na usimamizi kwa ulimwengu wote. Ndiyo sababu ushirika huu unapaswa kubaki umeungana na na mahali patakatifu" [*E. Viganò, Letter to the Rector of the Sanctuary of Mary Help of Christians in Turin, 24* July 1989].

Kila ushirika wa mashinani, kwa hivyo, unapaswa kutengeneza ushirika wa maelewano na umoja kwa mahali patakatifu pa Maria Msaada wa Msaada wa Wakristo kule Torino – *Valdocco* na hasa na ushirika wa kwanza ulioanzishwa kule; Ushirika ulio makao makuu utatekeleza wajibu wake kwa ajili ya muungano.

***Kipengee 10***

*Ushirika wa pekee katika maisha ya Chama*

Wakatoliki wote waliobatizwa hasa kuanzia miaka 18 wanaweza kujisajili kwa uwanachama katika ushirika huu.

Uanachama unadai jukumu la kuishi yote yaliyotajwa katika kipengee 4 cha sheria za sasa na pia kushiriki mara kwa mara katika vikao vya ushirika kwa roho ya umoja na pia uanachama.

Usajili wa mkandidati katika ushirika ni lazima iidhinishwe na rais pamoja na baraza lake. Hiyo hufanyika baada ya maandalizi ya kutosha ambayo si chini ya mwaka mmoja, na vikao vya kila mwezi.

Mkandidati aonyeshe uaminifu kwa ushirika wakati wa sherehe saa ya Maria Msaada wa Wakristo, na atapata cheti, sheria na beji ya uanachama.

Ushirika wa mashinani, ni lazima uangalie malezi endelevu ya wanachama, wapange shughuli zao kadiri ya mazingira yao wakifuata sheria.
Katika roho ya umoja na uanachama, kila mmoja anachangia matoleo kwa uhuru wake ili kukidhi mahitaji ya ushirika mahali alipo na pia kupitia mpango wa kanda, ambayo inachangia pia mahitaji ya ushirika katika makao makuu.

### *Kipengee 11*

*Nafasi ya uanachama*

Kwa ajili ya ushirika, na kuendeleza malezi, kwa kubadilishana hali ya maisha, ushirika wa mashinani unapanga yafuatayo:

- *Vikao vya kila mwezi (pia wafuasi wengine wa Familia ya Waselesiani wanaweza kushiriki bila pingamizi lolote) kwa ajili ya malezi ya kanuni, sala na sherehe au kuabudu Ekaristi Takatifu ikiwezekana tarehe 24 kila mwezi, siku ambayo Bikira Maria anakumbukwa kwe heshima.*
-*Siku ya Maria ya kila mwaka;*
- *Kushiriki katika sherehe au vikao vya Familia ya Waselesiani.*
- *Mazoezi ya kiroho kwa ajili ya wafuasi;*
- *Maandamano, hija, siku za ritriti au mfungo;*
- *Vikao vingine ambavyo vimepangwa na ushirika mahalia*.
- **Taz. Kipengee 4**

### *Kipengee 12*

*Baraza la utawala wa kituo katika ushirika*

Kila baraza la utawala wa kituo unaratibishwa na baraza, lililochaguliwa na wanachama wote kutoka orodha ya wanachama ambao wamejitangaza kuwa watakuwa tayari kuhudumia kwa udungu.
Baraza la utawala mahali, linahusu, raisi, makamu wa rais, mweka hazina, katibu, na baraza la wajumbe, kadiri ya mahitaji ya ushirika. Mlezi wa kiroho, mwanamume au mwanamke, pia ni mfuasi wa baraza hilo.

Kwa mkandidati kusajiliwa, anahitaji kura za wachache.
Wajumbe wa baraza wanabakia ofisini kwa kipindi cha miaka minne na wanaweza kuchaguliwa kwa miaka mingine minne.
Wakati baraza limekamilika, kazi za pekee ndani yake huamuriwa na baraza.

Rais ndiye huitisha vikao vya baraza na ndiye anaendesha; anatayarisha agenda na kuwasilisha kwa wajumbe wa baraza kupitia katibu. Rais anawakilisha ushirika katika vikao vya nje na hasa vikao vinaovyo husu vikundi vingine.

Makamo wa raisi, anachukua nafasi ya raisi wakati labda hana nafasi ya kuhudhuria vikao kwa sababu ambazo haziwezi kuepukika, hii hufanyika tu baada ya maelewano na raisi.
Mweka hazina anatunza mali ya chama kulingana na sheria za nchi husika na pia kwa maamuzi ya baraza. Kila mwaka huwakilisha matumizi ya fedha na bajeti.
Katibu, kwa maongozi ya rais, anawatumia wajumbe tarehe na agenda za mikutano, anaandika , na anatunza hifadhi ya ushirika.
Kwa kila mjumbe wa baraza, anapewa jukumu fulani mahali alipo kwa ajili ya ushirika.
Kwa kawaida baraza hukutana mara moja kwa mwezi.

***Kipengee. 13***

*Wanaoongoza katika maswala ya kiroho*

Walezi wa kiroho wa ushirika wanachaguliwa na Mkuu wa Waselisiani katika kanda au na Mkuu wa Mabinti wa Maria Msaada Wa Wakristo. Hao wanaendesha, kipekee malezi ya kiroho ya Waselesiani na ushirika katika maisha na miradi ya kanisa mahalia.
Wale amabo wanaweza kuchaguliwa kwa malezi ya kiroho ya wanachama, waweza kuwa kati ya wanachama wenyewe ikiwa wameandaliwa.

***Kipengee 14.***

*Mkuu wa Shirika na baraza la kitaifa.*

Ikiwezekana, katika ngazi ya juu ya shirika kwaweza kuwa mjumbe mmoja ambaye anaratibisha na kuongoza mabaraza ya wajumbe mashinani na Familia ya Waselisiani.
Baraza katika ngazi ya juu ya kanda huchaguliwa na marais wa mashinani. Muundo wake ni kama ifuatavyo: Rais, Makamo wa rais, Katibu, Mweka hazina, na baadhi ya wajumbe kadhaa.
Wajumbe wa baraza wanachaguliwa kwa miaka 4 na wanaweza kuchaguliwa tena kwa awamu ya pili miaka 4.
Mratibu wa kiroho, mke au mume, ni mjumbe wa baraza hilo.
Mahali inapowezekana, muundo wa waratibu wanaweza kuanzishwa.

### *Kipengee 15*

*Wajibu wa Makao Makuu ya Chama*

Ushirika wa Maria Msaada wa Wakristo umehusishwa na mahali patakatifu pa Maria Msaada wa Wakristo Torino – *Valdocco*, ambaye ndiye mrithi na mwendelezaji wa ushirika huu ulioanzishwa na Don Bosco mwenyewe, na ndivyo unaitwa "msingi".
Kwa sababu ya asili yake na kushirikishwa na mahali patakatifu, ushirika huu una wajibu wa kupyayusha, kuunganisha na kutoa habari kuhusu ushirika huu ulimwenguni.
Ndio maana inakua kiungo maalum cha Maria Msaada wa Wakristo, ambayo inachapishwa na jarida la "*Maria Ausiliatrice*", huko Torino.

### *Kipengee 16*

*Baraza la Ulimwengu la Ushirika*

Ni wajibu wa rais wa makao makuu ya ushirika kuitisha kikao cha Baraza la Ulimwengu la Ushirika.
Baraza hili linahusu wafuatao: Makamu wa Mkuu wa Shirika la Waselisiani, mjumbe wa Shirika la Mabinti wa Maria Msaada wa Wakristo kutoka ngazi ya juu ambaye ndiye kiungo na Familia ya Waselisiani, Rais na mratibu wa maisha ya kiroho na mjumbe

kutoka makao makuu ya ushirika, pamoja na wawakilishi wa nafasi zingine.
Kwa hiyo walei watakiwa kuwa wengi mno kuliko mapadre na watawa.
Baraza hili hukutana kila baada ya miaka 6: Katika nyakati maalum ya kongamano la Maria Msaada wa Wakristo, ambayo inapangwa na baraza la wajumbe wa makao makuu ya Ushirika.

***Kipengee 17.***

*Mali za Ushirika*

Ushirika wa Maria Msaada wa Wakristo, kwa sababu ni chama cha Kanisa kinachotawaliwa na sheria, kinaweza kuwa na mali, kutunza na pia kutumia kadiri ya sheria za Kanisa na sheria za nchi husika.

***Kipengee cha 18***

*Utafisiri wa Sheria*

Utafsiri wa sheria kwa lugha zingine ni lazima ufuate maandishi haya ya kisasa na tena utume Makao makuu kwa kuhakikisha.

## NYONGEZA 1

### KIGEZO CHA MKUSANYIKO WA WALEI KANISANI

(*Christifideles Laici n. 30*)

Daima ni kutoka kwa mtazamo wa ushirika wa Kanisa na utume, na si kinyume na uhuru wa kujiunga, hivyo mtu anaelewa umuhimu wa kuwa na vigezo wazi na wazi kwa kutambua makundi hayo yaliyowekwa, pia huitwa "*Vigezo wa Ufalme* ". Vigezo vya msingi vinavyofuata vinaweza kusaidia katika kutathmini chama cha waaminifu katika Kanisa:
- Uwezo unaotolewa kwa wito wa kila Mkristo kwa utakatifu, kama ilivyo imeonyeshwa "katika matunda ya neema ambayo roho hutoa kwa kila mwaamini "[LG 39] na katika ukuaji kuelekea ukamilifu wa maisha ya Kikristo na ukamilifu wa upendo [LG 40]. Katika maana hii chama chochote cha waamini;

daima huitwa kuwa chombo zaidi kinachoongoza kwenye utakatifu Kanisa, kwa kuimarisha na kukuza "umoja zaidi wa karibu kati ya maisha ya kila siku ya wanachama wake na imani yao "[AA 19].
- Wajibu wa kudai imani ya Kikatoliki, kukubaliana na kutangaza ukweli kuhusu Kristo, Kanisa na ubinadamu, katika kutii *Magisteriam* ya Kanisa, kama Kanisa linalitafsiri. Kwa sababu hii kila ushirika wa waamini wafuasi lazima uwe jukwaa ambapo imani inatangazwa pamoja na kufundishwa katika maudhui yake yote.
- Shahidi wa ushirika wa nguvu na wa kweli katika uhusiano na Papa, kwa kuzingatia kabisa imani kwamba yeye ni kituo cha daima na kinachoonekana cha umoja wa ulimwengu wote Kanisa [LG 23], na kwa Askofu wa ndani, "kanuni inayoonekana na msingi wa umoja "[LG 23] katika Kanisa fulani, na" kwa pamoja heshima kwa aina zote za utume wa Kanisa "[AA 23]. Ushirika na Papa na Askofu lazima waonyeshe kwa uwaaminifu utayari wa kukubali mafundisho ya mafundisho na mipango ya wachungaji wa Papa na Askofu. Aidha, ushirika wa Kanisa unahitaji wote kutambua aina nyingi za halali katika vyama vya waamini katika Kanisa na wakati huo huo, nia ya kushirikiana katika kufanya kazi pamoja.
- Kukubaliana na kushiriki katika malengo ya kitume ya Kanisa, yaani, "uinjilisti na utakaso wa ubinadamu na
Kuundwa kwa Kikristo kwa dhamiri ya watu, ili kuwawezesha kuifanya roho ya injili katika jamii mbalimbali na
nyanja za maisha "[AA 20]. Kwa mtazamo huu, kila aina ya aina ya kuweka waamini unaulizwa kuwa na bidii ya umisionari ambayo itaongeza ufanisi kwa washiriki katika uinjilisti tena.

- Kujitolea kwa uwepo katika jamii ya wanadamu, ambayo inaelekea Mafundisho ya Kanisa ya kijamii, huiweka katika huduma ya jumla heshima ya mtu. Kwa hivyo, vyama vya waamini vyapaswa kuwa na matunda ya ushirikiano katika kuleta hali kwamba ni haki zaidi na upendo ndani ya jamii. Vigezo vya

msingi vilivyotajwa wakati huu kupata ukaguzi wao katika matunda halisi ambayo fomu mbalimbali za kikundi zinaonyesha ndani ya maisha ya shirika na kazi wanazofanywa, kama vile: rejea upya kwa maombi, kutafakari, liturujia na maisha ya sakramenti, ufufuo wa wito kwa Wakristo wa ndoa, ukuhani wa utumishi na maisha ya kujitolea; utayari wa kushiriki katika mipango na shughuli za Kanisa katika ngazi za mitaa, kitaifa na kimataifa; kujitolea kwa nguvu na uwezo wa kufundisha na kuunda Wakristo; tamaa ya kuwa kuwasilisha kama Wakristo katika mazingira mbalimbali ya maisha ya kijamii na uumbaji na kuamka kwa kazi za usaidizi, utamaduni na kiroho; roho ya kikosi na umaskini wa kiinjili inayoongoza zaidi na ukarimu katika upendo kwa wote; uongofu kwenye maisha ya Kikristo au kurudi kwa ushirika wa Kanisa kwa wanachama waliobatizwa ambao wameanguka mbali na imani.
(*Apostolic Exhortation, 30/12/1988 of John Paul II, n.30*)

## NYONGEZA II

### MSAMAHA

Mungu hutoa msamaha kwa Kiburi cha dhambi iliyotendwa ambayo hatia tayari imesamehewa, waamini ambao wamewekwa vizuri na kwa hali fulani wanaweza kupata kupitia kuingilia kwa Kanisa ambalo, kama chombo cha ukombozi, lina mamlaka na kutumia hazina ya kuridhika iliyofanywa na Kristo na watakatifu.
Kiburi ni sehemu ya kawaida ya dhambi kwa vile inaelekeza mtu katika adhabu ya dhambi. Hakuna mtu anayeweza kuomba huruma kwa watu wengine ambao bado wanaishi. Huruma na msamaha wa kawaida inaweza pia kutumiwa kwa wafu kwa njia ya kutosha.

### MSAMAHA WA MUDA MREFU

Hati ya utume wa sheria ya tarehe tarehe 31 Januari 1968 ilitoa msamaha uliotolewa katika orodha zifuatazo katika nambari 1, na 4 hadi 10, na tarehe 6 Februari 2002 wale waliopewa 2 na 3, msamaha ulitolewa kwa muda mrefu.

1. Siku ya kujiunga na chama;
2. Mt. Fransisko wa Sale, 24 Januari;
3. Mt. Yohani Bosko, Januari 31;
4. Kupashwa habari Maria, Machi 25;
5. Maria Msaada wa Wakristo, Mei 24;
6. Hija, Mei 31;
7. Bikira Maria kupalizwa Mbinguni, Agosti 15;
8. Siku ya kuzaliwa kwa Mama yetu, Septemba 8;
9. Bikira Maria Imakulata, Desemba 8;
10. Siku ya Krismasi, Desemba 25.

**MASHARTI**

1. Kujitolea kupigana dhidi ya dhambi;
2. Kukiri kwa Sakramenti kwa Sakramenti ya Kitubio;
3. Ushirika wa Ekaristi;
4. Sala kwa madhumuni ya Papa;
5. Upyaji, angalau lakini waziwazi, ya ahadi ya kuzingatia kwa uaminifu Kanuni za Chama.

**N.B.**

a) Wajumbe wanaweza kupata kibali na msamaha wa muda mrefu kwa jumla kadiri ya siku zilizoorodheshwa, au siku ambayo sikukuu inahamishwa.

b) Wajumbe wanaweza kupata msamaha wa jumla kwa waamini wote katika kipindi cha mwaka wa Liturujia, lakini katika hali, ahadi ya kufuata kanuni haitajiki.

**MSAMAHA WA MUDA**

Kuna sala nyingi sana na matendo mema ambayo kwa kupata msamaha ni sehemu ya masharti.

Miongoni mwao ni mbili zilizopendekezwa na Don Bosco mwenyewe katika Kanuni za ADMA:

1. “*Isifiwe na itukuzwe sasa na siku zote Sakramenti Takatifu sana ya Kimungu*”.
2. *Maria Msaada wa Wakristo, tuombee.*

**Hali zingine tatu lazima pia ihifadhiwe katika akili; ni msamaha ambao unatolewa kwa waamini wote:**

1. Fadhila ya waamini ambaye, katika kutekeleza majukumu yao na kukabiliana na shida za maisha hujiaminisha kwa unyenyekevu kwa Mungu, na kuongeza wakati huo huo - hata kiakili - kuomba moyoni.

2. Kutoa fadhila kwa waamini ambao, kwa roho ya imani na huruma, hujiweka wenyewe na mali zao katika huduma ya ndugu au dada aliye na mahitaji.

3. Fadhila ya mwamini ambaye, kwa roho ya toba, kwa hiari hufanya malipizi kwa kitu halali.

## NYONGEZA III

## KANUNI YA WAFUASI WA MARIA MSAADA WA WAKRISTO

### Imeandikwa na Don Bosko

1. Katika Kanisa la Torino ambalo limewekwa kwa heshima ya Maria Msaada wa Wakristo, limewekwa rasmi na kisheria kwa idhini ya Askofu Mkuu wa Torino mfuasi wa Maria; Wajumbe wa Shirika hilo wanalenga kukuza heshima kwa Mama wa Mungu wa Mwokozi ili kustahili katika maisha na hasa wakati wa kufa.

2. Wao wana malengo mawili maalum: kueneza ibada kwa Bikira Maria na kumheshimiwa Yesu katika Ekaristi Takatifu.

3. Kwa hivyo watatumia maneno, ushauri, kazi njema na ushawishi wa kukuza utukufu na kujitolea katika karamu, sikukuu na maadhimisho yanayotokea wakati wa mwaka ili kumheshimu Bikira Mtakatifu na Sakramenti Takatifu Zaidi.

4. Kuenea kwa vitabu vyema, picha, medali na vipeperushi, kushiriki katika maandamano kwa heshima ya Maria mtakatifu sana na Ekaristi Takatifu kwa kuhimiza wengine kufanya hivyo, mara kwa mara kushirika na kuwepo kwa Misa takatifu, kuambatana na *Viaticum* kwa wanaokufa , ni mambo wanachama wanajaribu kukuza kwa njia zote zinazowezekana kwa hali yao katika maisha.

5. Wajumbe watajitahidi kamwe kutotumia lugha ya kashfa au kushiriki katika majadiliano kinyume na dini, na watajitahidi kabisa kuzuia wale walio chini ya malezi yao kufanya hivyo; wote wataondoa vikwazo katika njia ya utakaso wa siku za Jumapili na Siku ya Sikukuu.

6. Kila mwanachama, kulingana na ushauri wa Katekismui na wakurugenzi wa kiroho, amehimizwa vyema kupokea Sakramenti ya kitubio na Komunio mara moja kwa mara mbili au mara moja kwa mwezi, na kushiriki Misa ya kila siku ikiwa kazi yake inaruhusu.

7. Kila siku baada ya maombi yao ya asubuhi na usiku, wajumbe watasema kwa heshima ya Sakramenti Takatifu: "*Isifiwe na itukuzwe sasa na siku zote Sakramenti Takatifu sana ya Kimungu* "; na kwa heshima ya Bikira Maria: "*Maria Msaada wa Wakristo, utuombee*". Kwa makuhani inatosha katika misa kuwa na nia ya wafuasi wote wa ushirika. Sala hizi zitatumika kama dhamana ya kuunganisha wanachama wote ili wawe na roho moja na wazo moja kwa ajili ya kumwabudu Yesu aliyeko katika Ekaristi Takatifu na Mama yake, na kushiriki katika mema yote yanayotendwa na chama.

[*From "Letture Cattoliche", Year XVII, May, Vol. V, pp. 48-50*]

## IBAADA YA KUWAPOKEA WANACHAMA WAPYA

Aya no 10 ya sheria yatueleza kuwa: Mkandidati anaonyesha uaminifu kwa ushirika, katika sherehe kwa heshima ya Maria Msaada wa Wakristo. Baada ya homilia utaratibu huu ufuate:

*Kiongozi*:
Leo ni siku ya furaha kwenu ninyi mnao tazamia kujiunga na ushirika wa Maria Msaada wa Wakristo. Mmeomba kuwa wanachama wa ushirika huu ili kuwa mashahidi wa upendo kwa Bikira Maria Mtakatifu na wajibu wenu kumfanya atambulike na apendwe. Tuanze sherehe yetu kwa namna ya tendo la kawaida kwa kuwaita kila mmoja jina. Mwito huu una maana kwamba Maria Mtakatifu anawaalika kujiunga na ushirika ambao una jina lake.

*Kuwatambulisha Wakandidati*
Wakandidati wanaitwa na kiongozi wa ADMA, atawaita kwa majina yao yote. Na kila aliyehudhuria ataitika, "**Nipo**" na kujongea altare.

*MAHOJIANO*
***Kiongozi*:** Kadiri unavyojongea altare, unaomba nini?
***Wakandidati***: Tunaomba kuwa wafuasi wa Ushirika wa Maria Msaada wa Wakristo.
***Kiongozi*:** Je mnaelewa majukumu mnayochukua wenyewe kwa kujiunga na ushirika huu?
***Wakandidati*:** Kila mmoja binafsi atafanya maisha yake ya kiroho yawe mfano wa Bikira Maria, kuyafanya maisha yetu yawe kama yake, kumwamini Mungu pekee, na kufanya hii kuwa jukumu la maisha yote.
Hivyo, kusikiliza kama bikira alivyosikiliza, tutabaki makini kwa kusikiliza Neno la Mungu, ambalo tutatangaza kwa neno na mifano ya maisha yetu.

*Kama vile bikira alivyosali, tutahakikisha kuwa maisha yetu*

*yatanurishwa na sala ya rohoni katika mawazo na shukrani mbele ya Baba*. Kama Bikira Mama, tutashirikiana na Papa na maaskofu kwa ajili ya kukua kwa watu wa Mungu.
Kama vile bikira alivyojitolea mwenyewe, tutafanya maisha yetu matoleo kwa Mungu, kwa furaha ya kukamilishwa na mapenzi ya Baba ambayo ndiyo njia ya kutakatifuzwa.

*Kiongozi*: Ni majukumu yapi ya kipekee unayojiwekea kama mwanachama wa ushirika huu?
*Wakandidati*: Kama tabia yetu ya kipekee na wajibu, tunatazamia kueneza ibada kwa Maria Msaada wa Wakristo na kumwabudu Yesu katika Ekaristi Takatifu katika jamii yetu. Hayo yote tutatimiza kwa maneno yetu na matendo ambayo yanatokana na Injili na maisha ya kiroho na utume wa Mtakatifu Yohane Bosko.

**Baraka juu ya beji na kadi za uanachama:**
*Kiongozi*: Bwana unadhihirisha upendo wako ndani ya Bikira Maria, Mama yetu na msaada. Tunakuomba picha hizi, ziwe, ishara ya wokovu wako miongoni mwetu. Amina!
(*Kiongozi ananyunyizia maji ya Baraka*)
*Kiongozi:* Beji hizi zilizo na ishara picha ya Maria Msaada wa Wakristo zikukumbushe uanachama wako wa Ushirika wa Maria Msaada wa Wakristo ulionzishwa na Mt. Yohane Bosko. Maria Msaada wa Wakristo akuwezeshe kukuwa katika Bwana Yesu Kristo, kwa yule ambaye umechukua majukumu kuwa mfausi wake mwaminifu. Bikira Maria akupe ulinzi na usaidizi wa Mama. Amina!

**Kiapo wanachochukua Wakandidati**
**[***Wakandidati wote hupiga magoti na kusema yafuatayo***]**
Bikira Maria, Msaada wa Wakristo na Mama wa Kanisa, kwa kuwa mfuasi wa ushirika wako, ninaahidi kuwa shahidi mwaminifu wa Kristo katika maisha yangu ya kila siku, hasa kwa familia yangu, sehemu ya kazi, na katika jamii na Kanisa, kwa nguvu na uwezo unaotokana na sala, na katika kuopkea

Sakramenti ya Kitubio na Ekaristi mara kwa mara. Ninaahidi kuomba kwa ajili ya miito kwa ajili ya Kanisa na familia ya Kiselesiani, kwa kufuata mafundisho na mifano ya Mt. Yohane Bosko na kujiaminisha kwa msaada wa kimama utakao nipa.

*Wakristo wote hujibu*. Amina.

*Basi kila mwanachama hupewa katiba, beji na kadi ya uanachama.*

***Kiongozi:*** Sasa wewe ni mwanachama Kamili wa Ushirika wa Maria Msaada wa Wakristo, na mshiriki wa neema za kiroho za ushirika huu, na kazi zote njema zinafanywa ndani ya familia ya Waselesiani iliyoanzishwa na Mt. Yohane Bosko.
*Kiongozi:* Maria Msaada wa Wakristo.
*Wote wanaitikia: Utuombee*.

**SALA ZA WAAMINI**

***Kiongozi:***
Ndugu na dada, tumwombe Mungu Mwenyezi katika huruma yake, asikie sala tunazomtolea kwa maombezi ya Maria msaada wa Wakristo.
*Kiitikio*: **Bwana Utusikie**
1. Tunaliombea Kanisa Takatifu la Mungu, ili "Maria, Bikira mwenye nguvu, mtetezi wa Kanisa", alisaidie Kanisa kwa upendo wa kimama.
2. Tunaomba kwa ajili ya Baba Mtakatifu: Kama watangulizi wake Mt. Pio V na Pio VII apate ulinzi kamili wa Maria Msaada wa Wakristo katika majaribu yote na magumu katika Kanisa.
3. Kwa ajili ya maaskofu, mapadre na watawa, ili katika ushirika na Baba Mtakatifu, waongozwe katika imani na maisha ya Kikristo ambayo wamepewa kwa ajili ya kutunza na kulilinda Kanisa la Mungu.
4. Kwa ajili ya recta meja mkuu wa Waselisiani, na kwa wakuu na kamati mbalimbali za Familia ya Waselisiani, waweze kupata

ulinzi wa Maria Msaada wa Wakristo na Mt. Yohane Bosko katika shughuli zote za kuwaongoza Waselisiani.
5. Kwa ajili ya wote tulio hapa, wafuasi wa ushirika wa Maria Msaada wa Wkaristo, ulimwenguni kote na hasa kwa wale ambao wamekuwa wafuasi leo, kwamba katika kusherehekea na kuheshimu Maria Msaada wa Wakristo, tujisikie tumeungana katika sala na kuishi kwa kuendeleza ibada kwa Maria Msaada wa Wakristo, kwa ajili ya kutafuta miito mitakatifu kwa ajili ya Kanisa na Familia ya Waselisiani.

*Kiongozi:*
**Baba, ulimchagua Maria ashiriki katika mpango wako wa ukombozi wa Mwanadamu, sikiliza sala na maombi yetu ambayo tunakutolea katika imani, tunamwita yule ambaye umetupatia awe Mama na Msaada. Kwa njia ya Kristo Bwana wetu**. Amina.

## NOVENA
## MAANA YA SALA YA NOVENA

Neno la Kilatini Novena humaanisha tisa. Novena ni siku tisa za sala au ibada katika dini ya Kikristo. Inahusu sala za mtu binafsi au jamii ya watu. Novena imepata maana mpya kuwa alama ya kumbukumbu ya maisha ya sala kwa ajili ya jambo fulani. Kabla ya Yesu kupaa mbinguni aliwaagiza Mitume wake wabaki Yerusalemu hadi atakapokuja tena. Mitume wa Yesu na Bikira Maria walisali kuanzia kupaa kwake hadi wakati wa Pentekoste. Inahesabika kuwa tangu kupaa hadi Pentekoste ilikuwa kibindi cha siku tisa. Hivyo basi novena katika maana yake Kikristo ni siku tisa za sala maalum kwa ajili ya kumwelekea Mungu kiroho kila siku [Matendo *ya Mitume 1:12-2:5*]. Novena huwa na lengo maalum la kumwomba Mungu. Katika nyakati hizo za novena, waweza kutoa maombi nia yako, kwa ajili ya jambo fulani. Zaidi sana mtu yule hushiriki novena yoyote, hupokea neema kwa ajili ya kumwabudu Yesu akisaidiwa kwa maombezi ya Bikira Maria na Watakatifu.

### FAIDA YA NOVENA

Kusali novena humsaidia mtu kukua kiimani na pia kupata neema za Mungu kwa ajili mahitaji fulani. Katika Ubatizo tumefanywa kuwa wana wa Mungu na katika imani tunamfikia. Hivyo basi, ukiwa na shida, hitaji lolote, magonjwa na mahangaiko yoyote, novena hukuwezesha kujipa hamu na nidhamu ya kusali kila siku. Hali hiyo hukupa heri na neema za Mungu kila siku. Maana mawasiliano yako na Mungu huwa yapo kila siku na ushirika huu, hukufaidi wewe mwanadamu kwa kuwa katika hali ya neema. Utajaliwa amani na furaha katika maisha.
Tunasali novena kwa kujiandaa kwa tukio kuu la kiibaada au siku kuu Mfano: Kristmasi, sherehe au sikukuu ya mtakatifu msimamizi wetu na pia novena waweza kusali kwa ajili ya shukrani kwa Mungu kwa ajili ya jambo fulani, au kwa ajili ya kujiandaa kwa tukio fulani: mfano mitihani, afya, kwa ajili ya mpango fulani ya familia na mengine mengi. Zaidi ya yote

novena hukuimarisha katika imani na maisha ya kiroho. Katika novena utapata neema nyingi za Mungu kwa ajili ya kukabiliana na hali zote za maisha bila kupoteza matumaini au kukosa amani.

## NAMNA YA KUJIANDAA KWA NOVENA

*Fuata hatua zifuatazo:*

i) Kuwa na lengo mahsusi la kumrudia Mungu katika imani yako.

ii) Kuwa na lengo maalum au nia ambayo wataka kusali kwa ajili yake.

iii) Katika siku hizo za Novena, shiriki sakramenti ya kitubio.

iv) Pokea Ekaristi Takatifu.

v) Unaweza kumshirikisha mtu yeyote awe rafiki wa sala katika novena yako.

vi) Maliza Novena yako kwa Misa Takatifu.

vii) Baada ya kumaliza novena fanya tendo la huruma kwa kuwasaidia wengine wamjue Mungu.

viii) Fanya tendo la ukarimu, kulisaidia Kanisa kwa sala, sadaka, michango na ustawi wa maendeleo ya Kanisa kwa jumla.

## WAJIBU WA MTU ANAYESALI NOVENA

Mtu yeyote anayesali novena, aonyesha shukrani kwa neema ambazo amepata kwa Mungu. Maana siku zote unazosali novena ni za neema. Baada ya kusali novena siku tisa, onyesha shukrani kwa Mungu kadiri ya uwezo wako kulisaidia Kanisa kwa namna ya matoleo na ukarimu na pia kuwa mfano mwema kwa jamii. Uwe kielelezo cha imani. Novena haichukui nafasi ya majukumu ambayo wapaswa kutenda, bali inakupa neema ya kujipa matumaini na kuunganika na Mungu.

**Ni chaguo lako kufuata novena yeyote, maana lengo kuu la novena ni Shukrani kwa Mungu kwa neema ambazo tunapata na pia kudumu katika urafiki wake.**

Zifuatazo ni Baadhi ya Novena ambazo waweza kutumia katika kuimarika kiimani.

**1. NOVENA YA DAIMA KWA BIKIRA MARIA MSAADA WA WAKRISTO**

*Novena hii ni kama ilivyoshauriwa na Mtakatifu Yohane Bosko kwa ajili ya kupata neema na misaada ya Mungu.*

**KWA YESU KATIKA SAKRAMENTI YA EKARISTI TAKATIFU**

**Wote:** Ee Yesu mpendelevu sana – ambaye unapendezwa mno kukaa kati ya watu – na kuwa chakula cha roho zao – utusaidie tunakusihi- kwa njia ya mastahili ya Mt. Yohane Bosko – ambaye alijibidisha sana kuamsha katika vijana na Wakristu – tamaa ya kujiunganisha nawe mara nyingi- katika Sakramenti ya Ekaristi Takatifu- yaani Sakramenti ya upendo wako tuweze kupata tunaloomba kwa unyenyekevu na tamaa kubwa ya roho zetu.

*Salamu Maria x3……. Baba yetu x3…… Atukuzwe Baba x 3….”**Isifiwe na itukuzwe sasa na siku Zote Sakramenti Takatifu sana ya Kimungu”***

**KWA BIKIRA MARIA, MSAADA WA WAKRISTO**

**Wote**: Ee Bikira Mtakatifu sana msaada wa Wakristo – ambaye, kwa njia ya Mt. Yohane Bosko- ulitenda, na bado unaendelea kutenda miujiza mingi –utupatie twakusihi kwa wema wako wakimama-na kwa mastahili yake- sisi maskini wakosefu- tuweze kupata misaada tunayohitaji-ambayo tunaiomba-kwa tamaa kubwa ya roho zetu.

*Salamu malkia, mama mwenye huruma x3,…***Maria Msaada wa Wakristo utuombee**!

**KWA MTAKATFIU YOHANE BOSKO**

**Wote:** Nawe, Mt. Yohane Bosko uwatolee Yesu na Maria sala zetu – basi pamoja na neema tunaomba-pia utuwezeshe kwa maombezi yako – kupata na kuongezewa zaidi na zaidi- upendo

kwa Yesu katika Sakramenti ya Ekaristi Takatifu na kwa Bikira Maria Msaada wa Wakristo –Amina.

***Mt. Yohane Bosko Utuombee!***

**BARAKA YA BIKIRA MARIA MSAADA WA WAKRISTU**

**Padri:** Msaada wetu katika jina la Bwana.
**Wote:** Aliyeumba mbingu na dunia.
*Salamu Maria………………*
**Wote:** Tunakimbilia ulinzi wako Ee Mzazi Mtakatifu wa Mungu usitunyime tukiomba katika shida zetu utuopoe daima katika hatari zote ewe Bikira Mtukufu mwenye baraka.
**Padri:** Maria Msaada wa Wakristo!
**Wote:** Utuombee!
**Padri**: Ee Bwana usikilize sala yangu,
**Wote**: Mlio wangu ukufikie!
**Padri**: Bwana awe nanyi!
**Wote**: Awe pia nawe!

Tuombee
**Mungu Mwenyezi wa milele ambaye kwa msaada wa Roho Mtakatifu ulitayarisha mwili na roho ya Bikira Maria Mtukufu kuwa kikao kistahilifu cha mwanao utujalie kwamba kama tunavyosherehekea kwa furaha kumbukumbu yake tuweze kwa maombezi yake ya kipendo kutenganishwa na mabaya ya dunia hii na upotevu wa milele kwa njia ya Yesu Kristu Bwana wetu. Amina**!

**Padri:** Baraka yake Mungu Mwenyezi ya Baba na Mwana, na Roho Mtakatifu, iwashukie na kukaa nanyi daima. Amina!

**2. NOVENA YA EKARISTI KWA MARIA MSAADA WA WAKRISTO**

*Yohane Bosko alikuwa muenezaji mkuu wa ibaada kwa Maria Msaada wa Wakristo. Kwa wale wote waliomwomba msaada, aliwashauri wasali novena hii kwa Maria Msaada wa Wakristo.*

*Miujiza mingi ilitendeka kwa wale waliofuata ushauri wa Mtakatifu Yohane Bosko.*

i. Kwa siku 9 sali sala zifuatazo kwa heshima ya Yesu katika Ekaristi Takatifu, *Baba yetu…….. x3, Salamu Maria………. x 3, Atukuzwe Baba………….. x3 pamoja na sala fupi*; " **Isifiwe na itukuzwe sasa na siku zote Sakramenti Takatifu sana ya Kimungu**". Halafu sala ya *Salamu Malkia….x3* …pamoja na sala fupi: "**Maria Maria Msaada wa Wakristo utuombee**!

ii. Shiriki Sakramenti ya Kitubio kadiri ya mahitaji yako na Ekaristi Takatifu katika siku hizi za Novena. Kuwa mkarimu kwa kazi za Don Bosco kadiri ya uwezo wako kwa namna ya matoleo au mchango wowote.

**3. NOVENA KWA MARIA MSAADA WA WAKRISTO**

*Novena ifuatayo ni ile ndefu, kwa siku tisa. Utaratibu wake wa imbada upo baada ya Novena hii.*

## SIKU YA KWANZA

**UTII**

**KKK 2216-17; 2251; 411, 475, 532, 539, 612, 615, 908, 1009, 1269**

Katika maana na hali ya kawaida, utii ni kusikiliza na kutii amri kutoka kwa yule aliye mkuu na kufuata maagizo yake. Ukifuata utapata heshima na pia baraka. Ukikosa kusikia na kutekeleza utapata adhabu. Utii katika Maandiko Matakatifu, ni kusikiliza Neno la Mungu na kutimiza yale unayoambiwa. Ukiwa mtii kwa Neno la Mungu, basi una baraka, ukikosa wewe una laana. Utii katika Ukristo unamaanisha kusikia; kuamini; kujitoa kwa Mungu na Neno lake.

Bwana wetu Yesu Kristo alitupatia matumaini kuwa amefika hapa ulimwenguni si kufanya mapenzi yake bali mapenzi ya Baba yake. Tunasoma jinsi anavyoeleza mwenyewe:

“ *Kwa kuwa mimi sikushuka kutoka mbinguni ili niyafanye mapenzi yangu, bali mapenzi yake aliyenipeleka. Na mapenzi yake aliyenipeleka ni haya, ya kwamba katika wote alionipa nisimpoteze hata mmoja, bali nimfufue siku ya mwisho. Kwa kuwa mapenzi yake Baba yangu ni haya, ya kwamba kila amtazamaye Mwana na kumwamini yeye, awe na uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho*”[ Yoh 6:38-40]

Maisha yake Yesu yalikuwa utii kwa Baba. Yeye alijulikana kama Mwana na Mtumishi kuonyesha kwamba alikuwa na umoja na Baba kwa kumtii. Utii unamfanya kuwa tayari katika kazi ya utume – kuwakomboa watu. Kuwa mfuasi wa Kristo utii ni muhimu humpa mtu heri kwa kumtayarisha kwa ajili ya utume ambao ameitwa kutekeleza. Utume huo ni lazima uwe na majukumu yanayodai ukarimu na moyo wakujitolea.
Roho ya utii yapaswa yafuatayo:

- *Kuishi imani kikamilifu.*
- *Ni kuweka maanani katika jambo linalompendeza Mungu Baba na kuwachana na mambo ya tamaa ambayo yanakupendeza wewe na kukufanya uwe mbinafsi na mnafiki.*
- *Kutafuta mapenzi ya Mungu Baba kwa njia ya sala, utume, kutafuta ushauri na kufuata ishara ambazo Mungu anatujalia.*
- *Kukubali kwa hiari imani tuliyopewa na kutafuta utakatifu katika maisha ya kila siku. Kukubali mafundisho na mwongozo wa viongozi wa Kanisa hasa baba mtakatifu, maaskofu na mapadre. Kufuata amri kumi za Mungu na amri za Kanisa.*
- *Kutimiza wajibu wako kila siku Kwa ubunifu na ukarimu, kutumia muda wako kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Kujitolea kwa hali na mali katika kusitawisha Kanisa kwa kuwa mkarimu.*
- *Kuwa mvumilivu nyakati za shida kwa kumwangalia Yesu Kristo Msalabani.*

Sote tuu washiriki wa Kanisa, mbatizwa hawi wake yeye mwenyewe bali wa yule aliyekufa na kufufuka kwa ajili yetu. Toka hapo umeitwa kujiweka chini ya wengine, kuwatumikia katika umoja wa Kanisa na kuwa "**mtii**" na "**mnyenyekevu**" kwa viongozi wa Kanisa na kuwaheshimu na kuwapenda. Sawa kama Ubatizo ulivyo asili ya uwajibikaji na majukumu, vivyo hivyo mbatizwa hufurahia haki katika Kanisa: kupokea Sakramenti, kulishwa Neno la Mungu na kusaidiwa na misaada mbalimbali ya kiroho ya Kanisa [KKK 1269].

Uhai, uwezo na vipaji tulivyo navyo Mungu anatuita tuvitumie kwa ajili ya wengine. Japo huwa jambo gumu, lakini tunao mfano dhabiti wa kimsingi kutoka Mwana wa Mungu.

## SABABU MUHIMU KUMTII MUNGU

### 1. Yesu atualika kuwa watii

Yesu Kristo ndiye mfano bora wa utii. Kama wafuasi wake ni lazima kufuata mfano wake na amri zake. Sababu kuu ya kuwa watii ni kama ifuatavyo:
"*Mkinipenda mtazishika amri zangu*"[Yoh 14:15]

### 2. Utii ni Ishara na alama ya Ibada

Ukombozi ni zawadi ya Mungu mwenyewe, kwa namna zetu wenyewe hatuwezi kumiliki. Utii wa kweli wa Mkristo hutokana na hali yake ya shukrani na neema ambayo imetoka kwa Mungu.

*"Basi ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana*" [*Rum 12:1*].

**3. Mungu huzawadia Utii**

Katika maandiko Matakatifu tunasoma kuwa Mungu hubariki mtu yeyote ambaye anatii.
"*…na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watajibarikia; kwa sababu umetii sauti yangu*"[ Mwa 22:18];Mwa 22:18; Kutoka 19:5; Luka 11:28; Yakobo 1: 22-25

**4. Utii kwa Mungu ni ishara ya Upendo wetu kwake**

"*Katika hili twajua kwamba twawapenda watoto wa Mungu: tumpendapo Mungu, na kuzishika amri zake"[ 1 Yoh 5:2-3]; 2 Yoh 6*

**5. Uti kwa Mungu ni alama ya Imani**

"Na katika hili twajua yakuwa tumemjua yeye, ikiwa tunashika amri zake. Yeye asemaye, "Nimemjua," wala hazishiki amri zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake. Lakini yeye ashikaye neno lake, katika huyo upendo wa Mungu umekamilika kweli kweli. Katika hili twajua ya kuwa tumo ndani yake. Yeye asemaye ya kuwa anakaa ndani yake, imempasa kuenenda mwenyewe vilevile kama yeye alivyoenenda.

**6. Utii ni afadhali kuliko Sadaka**

[*1 Sam 15:22-23*]

**7. Kutotii humwelekeza mtu katika dhambi na kifo**

Kutotii kwa Adam kulileta dhambi na kifo katika ulimwengu. Utii wa Kristo ulileta ushirika na Mungu kwa wale wanao mwamini.

Kwa sababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja, watu wengi walingizwa katika hali ya wenye dhambi, kadhalika kwa kutii kwake mmoja watu wengi wameingizwa katika hali ya wenye haki *[Rum 5:19*; *1 Kor 15:22]*

**8. Katika Utii, tunapata baraka takatifu katika maisha**

Ni Yesu pekee aliye mkamilifu, ni yeye tu aliyeweza kuwa na utii kamili. Tukimkubali Roho Mtakatifu kutuongoza na kutubadirisha kutoka ndani mwetu, tunaanza kukua katika utakatifu.

Heri walio kamili njia zao; waendao katika sheria ya Bwana….[*Zab 119:1-8*], *Isaya 48:17-19; 2 Kor 7:1*]

**Tafakri ya Maandiko Matakatifu**

*Wafilipi 2:1-11, Zab 40*

**Tuombe**

Bikira Mtakatifu

, Msaada mkubwa wa Wakristo, nakuelekea katika imani. Katika huruma yako sikiliza sala yangu mimi mdhambi maskini, nina kuomba msaada wako nishinde dhambi na kuepuka mazingira yake.

*Baba yetu….x3; Salamu Maria…x3; Atukuzwe Baba….x3 Salamu Malkia…..*

## SIKU YA PILI

**Ufukura**

"*Ukitaka kuwa mkamilifu, enenda ukauze ulivyo navyo, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuate*"[*Mt 19:21*]

Yesu alichagua hali ya ufukara kuwa njia yake ya utume na ukarimu. Alijitolea sadaka na kutimiza mapenzi ya Baba. Nasi

tupate utajiri wetu mkuu kwa ajili ya ukarimu kwa wahitaji. Ufukara ni hali ya moyo na jambo la kitume. Ni hali ya maisha ambayo yanamweka mtu huru na tayari katika utumishi. Ufukara huu, sio ule umaskini; ni hali ya roho ya kumchagua Mungu dhidi ya vitu vyote vya ulimwengu. Ufukara hutuwezesha kuchagua mambo adili na wema wa jumuiya, kama haki na usawa wa watu wote katika jamii.

**Mambo yafuatayo yaweza kumsaidia mtu kukua katika wema**:

- *Kufuata mfano wa Yesu wa ufukara na kupata hazina kuu.*

*"zaidi ya hayo nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu; ambaye kwa ajili yake nimepata hasara ya mambo yote nikiyahesabu kuwa kama mavi ili nipate Kristo"[ Wafilipi 3: 8]*

- *Ufukara Ni kuishi maisha ya kawaida, bidii na furaha katika utendaji bila kujitakia makuu, kupenda wito wa kutumikia na siyo kutumikiwa na kufanya majitoleo kwa ajili ya wengine.*
- *Kumwamini Mungu kuwa Yeye ndiye anaongoza maisha yako na kukupa kila kitu chema. Kutumia uhai ulio nao vema na kuwa mkarimu kwa vitu vyote Mungu amekujalia kupata katika maisha.*
- *Katika msingi wa imani uliopokea; ni kupenda kuwa mkarimu na kuwasaidia wale ambao wana hali duni ya maisha.*

Katika ufukara kila mmoja huweka wazi uwezo wake wa vitu, mali, muda, elimu na ujuzi, na maisha ya kiroho kwa ajili ya utukufu wa Mungu kwa kuwahudumia wengi na utume wa Kanisa na kazi zake. Tunatambua ukarimu wa Bwana wetu Yesu Kristo: Japo alikuwa tajiri alijifanya fukara ili sisi tuwe tajiri [2 **Kor 8:9**]. Tunaamua kumfuata mkombozi ambaye alizaliwa katika ufukara, ambaye hakumiliki kitu chochote na akafa msalabani akiwa nusu uchi.

Bwana wetu Yesu Kristu, anatualika kuwa huru kutokana na wasiwasi na mahangaiko ya vitu vya ulimwengu. Anataka

tumwamini katika ufadhili wake na ufadhili wa Mungu Baba. Twapaswa kujitolea kutangaza habari njema ya Injili [Mt *6:25*].

Wakristo wa Kwanza walituwekea mfano tayari wa ukarimu katika kushirikishana vitu vya ulimwengu huu. Nasi tumepewa vipaji vingi na Mungu kwa ajili ya ukarimu huo.

**Tafakari ya Maandiko Matakatifu**
*Matendo ya Mitume 4:32-37; Zab 103*

**Tuombe**
**Ewe Bikira Maria Mtakatifu, Mama mwenye huruma na neema, kwa msaada wa kweli umewaokoa Wakristo kutoka mashambulizi ya adui, nakuomba uilinde roho na mwili wangu dhidi ya mashambulizi ya muovu wa ulimwengu huu,ili niwe mshindi dhidi ya maadui wa roho yangu. Amina!**
*Baba yetu….x3; Salamu Maria…x3; Atukuzwe Baba….*
*Salamu Malkia*

## SIKU YA TATU

### Usafi wa Moyo

"*Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba , wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza* kututenganishwa *na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Bwana wetu*"[ Rum 8:38-39]

Usafi wa moyo ni kukamilisha ujinsia ndani ya mtu. Ni pamoja na majifunzo ya kujitawala nafsi [KKK 2395]
Usafi wa moyo ni zawadi ambayo Mungu hutujalia kwa sababu ya Ufalme wa Mungu. Katika imani tunakubali kwa shukrani na tunajiweka katika namna ya kuishi kiaminifu. Tumfuate Yesu

Kristo kiaminifu kwa kuchagua njia ya mapendo kumpenda Mungu na jirani kwa moyo wote.
Tuishi maisha yetu kwa ajili ya upendo wa Mungu na upendo wa wanadamu usio na mipaka. Twapaswa kuwapenda vijana na watoto wanaokuwa kwa kuwaonyesha wema wa Mungu na ndio maana ya malezi. Namna ya kukua katika usafi wa moyo:

- *Upendo ndio msingi wa maisha ya mwanadamu. Upendo hauhusu tu kimwili bali pia maisha ya kiroho na kimwili. Tuelewe kuwa upendo kamili ni kwa ajili ya mwingine. Ni zawadi ambayo humwezesha mtu kujinyima na kufanya majitoleo.*
- *Kumpenda Mungu kwa roho na nguvu zako zote katika kupenda wito wako na kuwatumikia wengine.*
- *Ni vema kuelimika katika ukarimu na upendo kwa ajili yaw engine. Hii inahusu ukweli, haki, uaminifu, urafiki, kuelewana na kushinda vikwazo vyote dhidi yake.*
- *Ni vema kuelewa udhaifu wako Ili ujiwekee njia ya kinga, Kwa kuweza kutawala vionjo, kuwa mwangalifu katika uhusiano na urafiki na kutumia vema vyombo vya mawasiliano na mitandao.*
- *Kumwomba Mungu msaada wake na neema, ili kumpenda sana Kristo. Kushiriki Sakramenti ya Kitubio kama namna ya kujitakasa na kumpenda Mama Bikira Maria.*

Usafi wa moyo ni fadhila ya maadili. Pia ni kipaji kutoka kwa Mungu, ni neema, ni tunda la juhudi za kiroho. Roho Mtakatifu humwezesha mtu ambaye maji ya ubatizo yamemzaa mara ya pili kuiga usafi wa Kristo [*KKK 2345*].
Wabatizwa wote wanaitwa kuwa na usawi wa moyo. Mkristo ‘amemvaa Kristo”, kielelezo cha usafi wa moyo. Waamini wote katika Kristo wanaitwa kuishi maisha ya usafi wa moyo kufuatana na hali zao za pekee katika maisha. Wakati wa Ubatizo wake Mkristo anajikabidhi kuishi hisi zake katika usafi wa moyo [*KKK 2346*]

**Tafakari ya Maandiko Matakatifu**
*Rum 8:35-37 au 2 Kor 10:17-11.2; Zaburi 11*

**Tuombee**
**Maria Malkia mwenye nguvu, Ni wewe pekee ulishinda uzushi ambao ulitaka kuligawanya Kanisa, nisadie, nakuomba nishike imani yangu na uniokoe na vitisho na mafundisho potofu. Amina!**
*Baba yetu….x3; Salamu Maria…x3; Atukuzwe Baba….x3 Salamu Malkia…..*

## SIKU YA NNE
### Sakramenti ya Ekaristi
**"***Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu anao uzima wa milele, nami nitamfufua siku ya mwisho [Yoh 6:54]*

Kanisa latufundisha kuwa, Ekaristi ni "*chemichemi na kilele cha maisha yote ya Kikristo*" .Katika Ekaristi takatifu mna kila hazina ya kiroho ya Kanisa, yaani Kristo mwenyewe, "Pasaka wetu". Ekaristi ni kilele cha tendo la Mungu la kuutakatifuza ulimwengu katika Kristo, na kilele cha tendo la kumwabudu Mungu wampalo watu Kristo, na kwa njia yake wampalo Baba katika Roho Mtakatifu.

**Ekaristi Ni tendo la shukrani na masifu kwa Baba**
- *Ni sakramenti ya wokovu iliyotekelezwa na Kristo Msalabani, ni pia sadaka ya sifa katika shukrani kwa ajili ya kazi ya uumbaji. Katika sadaka hii, kila kiumbe kinachopendwa na Mungu hutolewa kwa Baba kwa njia ya kifo na ufufuko wa Kristo.*
- *Kwa njia ya Kristo, Kanisa latoa sadaka ya sifa katika shukrani kwa ajili ya kila kitu ambacho Mungu amekifanya chema, kizuri, Na sawa, katika uumbaji na katika binadamu.*
- *Ekaristi Ni sadaka ya shukrani Kwa Baba, Ni Baraka ambayo kwayo Kanisa huonyesha shukrani yake Kwa Mungu Kwa*

*ajili ya fadhili zake zote, Kwa ajili ya kila kitu ambacho amekifanya Kwa njia ya uumbaji, ukombozi na utakaso. Mhali pa kwanza, Ekaristi ni "shukrani".*

- *Ekaristi ni sadaka ya sifa, kwa hii Kanisa huimba utukufu kwa Mungu kwa jina la viumbe vyote. Sadaka hii ya sifa yawezekana tu kwa njia ya Kristo.*

**Matunda ya Komunyo Takatifu**

- **Komunyo Takatifu huukuza muungano wetu na Kristo**: Tunda la msingi la kupokea Komunyo takatifu ni umoja wa ndani na Kristo. Yeye mwenyewe husema:

*"Aulaye mwili wangu ma kuinywa Damu yangu hukaa ndani yangu, nami hukaa ndani yake"[Yoh 6*:56]

- **Komunyo takatifu yatutenga na dhambi**: *Mwili wa Kristo tunaoupokea katika komunyo takatifu, "hutolewa kwa ajili yetu" na damu tunayokunywa "inamwagika kwa ajili ya wengi kwa maondoleo ya dhambi." Kwa sababu hiyo Ekaristi Takatifu inatuunganisha na Kristo kwa sababu anatukinga na dhambi.*
- **Umoja wa Mwili wa Fumbo: Ekaristi inaunda Kanisa.**

*Wanaopokea Ekaristi huunganishwa kwa ndani Sana na Kristo. Kwa njia yake Kristo huwaunganisha hawa na waamini wote katika mwili mmoja: Ndilo Kanisa*.[ 1 Kor 12:13; 1 Kor 10:16-17]

- **Ekaristi yatufanya tujitoe mhanga kwa maskini**: *Ili kupokea katika kweli Mwili wa Kristo na Damu ya Kristo iliyotolewa kwa ajili yetu, lazima kumtamani Kristo ndani ya ndugu zake walio fukara sana.*

**Kuabudu Ekaristi**

Katika Misa twaonyesha imani yetu kwa uwepo wa Kristo chini ya maumbo ya mkate na divai, kati yam engine, kwa kupiga magoti au kwa kujiinamisha kifudifudi kama ishara ya kumwabudu Bwana. "Kanisa Katoliki daima lilitoa na linaendelea kutoa ibada ya kuabudu inayostahili Sakramenti ya Ekaristi, sit u wakati wa Misa pia nje ya adhimisho lake: Kwa

kuhifadhi kwa uangalifu mkubwa sana hostia zilizogeuzwa, kwa kuziweka mbele ya waamini ili waziabudu kwa heshima kubwa, wakizichukua katika maandamano.
Kristo amependa awemo katika Kanisa lake kwa namna ya pekee. Kwa kuwa Kristo alikuwa anawaacha walio wake wasimwone tena kimwili, alipenda kutupatia uwepo wake kisakramenti; na kwa kuwa alikuwa anaend kujitoa msalabani ili kutuokoa, alitaka sisi tuwe na kumbukumbu ya upendo ambao kwao alitupenda hadi kutoa uzima wake.

**Tafakari ya Maandiko Matakatifu**
*Isa 25:6; 55:1-2; Zab 22:26; Mt 22:2-14; Lk 14:15; Ufu 3:20; 19:9; Yoh 19:36; 1 Kor 5:7, Rejea Sakramenti ya Ekaristi*

**Tuombee**
**Ewe Bikira Maria, Mama Mwema, Malkia wa Mashahidi, ujaze moyo wangu na nguvu za kuvumilia, nishinde ubinadamu wangu, ili niishi imani ya dini yangu, kikamilifu nyakati zote kama mtoto wako mwaminifu. Amina!**
*Baba yetu….x3; Salamu Maria…x3; Atukuzwe Baba….x3 Salamu Malkia…..*

## SIKU YA TANO

### Sakramenti ya Kitubio

"*Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni na kuiamini Injili*" [Mk 1:15]

Sakramenti ya Kitubio huleta huruma ya Mungu ambayo ni ondoleo la kosa lililotendwa dhidi yake, na papo hapo hupatanishwa na Kanisa ambalo dhambi yao imejeruhi, na ambalo kwa mapendo, mfano na sala huhangaikia wongofu wao.

Kwa njia ya Sakramenti za kuingizwa katika Ukristo, mtu hupokea uzima mpya wa Kristo. Lakini twauchukua uzima huu katika "vyombo vya udongo" nao hubaki "umefichika pamoja na Kristo". Tumo bado katika "makao ya duniani" tukielemewa na hali ya mateso, magonjwa na kifo. Uzima huu mpya wa mtoto wa Mungu waweza kudhoofika na hata kupotezwa kwa dhambi.

**Namna mbalimbali za toba:**

- **Sala, Kufunga na sadaka:-** *Huu ni uongofu kuhusu mtu mwenyewe kwa kupata msamaha kutoka kwa Mungu. Ni juhudi zinazofanywa Ili kujipatanisha Na jirani, juhudi kwa ajili ya wokovu wa jirani.*
- *Maisha ya kila siku: Wongofu hufanyika Kwa matendo ya upatanishi, msaada Kwa maskini, kutenda Na kutetea haki Na sheria, kukiri makosa, kuonyana, kupokea mateso, kuvumilia madhulumu kwa ajili ya haki. Kubeba msalaba kila siku na kumfuata Yesu diyo njia ya hakika ya toba.*
- **Ekaristi na toba:** *Ekaristi huifanya iwepo sadaka ya Kristo iliyotupanisha na Mungu. Ekaristi ni kinga inayotuokoa na makosa yetu ya kila siku na hutukinga na dhambi za mauti.*
- **Maandiko Matakatifu na sala ya Liturjia***: Kusoma maandiko Matakatifu, kusali sala ya Liturjia ya vipindi na sala ya Baba yetu, kila tendo nyofu la kumwabudu Mungu au uchaji huhuisha ndani yetu roho ya wongofu na ya toba na huchangia katika msamaha wa dhambi zetu.*
- **Nyakati na siku za toba***: Katika mwaka wa Liturjia [Kipindi cha Kwaresima, kila Ijumaa kukumbuka kifo cha Bwana] ni nyakati nzito za zoezi la toba ya Kanisa. Nyakati hizi za pekee zimewekwa Kwa ajili ya zoezi ya kiroho, liturjia ya toba, kuhiji Kama ishara ya toba, kujinyima Kwa hiari Kama kufunga Na kutoa sadaka, kushiriki kidugu kazi za mapendo na za kimisionari.*

**Matunda ya Sakramenti ya Kitubio:**

- *Upatanisho na Mungu*: Sakramenti hii hukurudisha katika neema ya Mungu, na kukuunganisha naye katika urafiki wa ndani. Inakuletea amani na utulivu wa dhamiri inayosindikizwa

na faraja kubwa ya kiroho. Hurudisha hadhi na mema ya maisha ya watoto wa Mungu, ambayo lililo na thamani zaidi ni urafiki wa Mungu.

- *Upatanisho na Kanisa:* Dhambi huharibu na kuvunja ushirika wa kidugu. Sakramenti ya Kitubio huutengeneza upya umoja huowa Kanisa.

**Tafakari ya Maandiko Matakatifu**
*Law 16:1; Ebr 9:6-14; Ayu 42:7-9; Isa 53:12; Rejea Sakramenti ya Upatanisho*

Tuombe
**Ewe Mama Bikira Maria, katika ushindi wa Papa Pius VII, umeonyesha, ulinzi wako mkuu, ulilinde Kanisa lote na kiongozi wake. Mlinde dhidi ya adui zake walio wengi, ili aweze kuendesha kazi aliyokabidhiwa Petro ya kulilinda Kanisa na kutunza imani yake. Amina!**
*Baba yetu….x3; Salamu Maria…x3; Atukuzwe Baba….x3 Salamu Malkia…..*

## SIKU YA SITA

**Sala**
**"***Hata alfajiri na mapema sana akaondoka, akatoka kaenda zake mahali pasipokuwa na watu, akaomba huko" [Mk 1:35]*

Sala ni "ukumbusho wa Mungu", ambayo ni kumbukumbu ya moyo. Mapokeo ya Kikristo yamehifadhi mitindo mitatu mikubwa ya maisha ya sala. Na yote ina tabia moja tu: Utulivu wa moyo.

**Sala ya Sauti**

- *Mungu anasema na mtu kwa njia ya Neno lake. Kwa njia ya maneno, ya akili au ya sauti sala yetu hutwaa mwili.*
- *Mungu huwatafuta wamwabuduo katika roho na kweli, na kwa hiyo sala ahia inayopanda vilindi vya moyo.*

- *Sala ya sauti ni sala ya vikundi kwa namna ya pekee. Sala huwa ya ndani kadiri tunavyomtambua yule ambaye "tunasema naye". Sala ya sauti huwa hatua ya kwanza ya sala ya tafakari.*

**Sala ya Fikara**

- *Fikara ni hasa kutafuta. Roho inatafuta kufahamu kwa nini Na jinsi gani ya maisha ya Kikristo, ili kushikamana na kujibu kile ambacho Bwana anataka.*
- *Tunasaidiwa katika sala ya fikara: kwa kusoma Maandiko Matakatifu na kutafakari juu yake. Au hata rozari inatuingiza katika maswala ya imani.*
-

**Sala ya Taamuli**

- *Sala ya taamuli ni sala ya moyo, inayouelekeza moyo wa mwanadamu kuwa na ushirika wa ndani na Mungu.*
- *Sala ya taamuli ni sala ya mtoto wa Mungu, ya mdhambi aliyesamehewa anayekubali kuyakaribisha mapendo ambayo kwayo anapendwa, na anayetaka kuyajibu kwa kupenda hata zaidi.*
- *Sala ya taamuli ni mtazamao wa imani uanomkazia macho Yesu. Ni kusikiliza Neno la Mungu. Ni sala ya ukimya ambao ni alama ya ulimwengu ujao.*
- *Sala ya taamuli ni uonyesho tu wa fumbo la sala. Ni mapendo ya kimya na inatufanya tushiriki fumbo la Kristo.*

**Tafakari ya Maandiko Matakatifu:**

Mt 14:23; Mk 1: 35; Mt 14:19; 15:36; Lk 23:34; Yn 17:9-24; Ebr 5:7; Zaburi 35; Zaburi 31;

Tuombe

**Ewe Bikira Maria, Malkia wa Mitume, walinde Maaskofu, mapadre na watoto wote wa Kanisa Katoliki,wape roho wa umoja, uti kamili kwa baba mtakatifu, na bidii kwa ajili ya wokovu wa wanadamu.Nakuomba uwalinde wamissionari, ili waweze kuleta kabila zote katika imani ya kweli ya kumfuata**

**Yesu Kristo!, ili kuwe na kundi moja la kondoo na mchungaji mmoja. Amina!**
*Baba yetu….x3; Salamu Maria…x3; Atukuzwe Baba….x3 Salamu Malkia…..*

## SIKU YA SABA

### Utakatifu

**"***Nena na mkutano wote wa wana wa Israeli, uwaambie, mtakuwa watakatifu; kwa kuwa mimi Bwana, Mungu wenu, ni mtakatifu***"[**Mambo ya Walawi 19:2**]**

Utakatifu ni sifa na hali ya Mungu anayeumba, ni sifa pia ya Yesu Kristo Mwana wa pekee wa Mungu anayekomboa, ni sifa na hali ya Roho Mtakatifu anayetakaza. Mungu Mwenyezi ametuumba katika utakatifu na ndivyo anaendelea kutoa mwaliko na mwito kila siku: Bwana akanenana na Musa, akamwambia, *"Nena na mkutano wote wana wa Israeli, uwaambie, Mtakuwa watakatifu, kwa kuwa mimi Bwana, Mungu wenu, ni mtakatifu*"..[Mambo ya Walawi 19:1-2]. Yesu pia alirudia haya maneno ya Baba kwa kusema, "*Basi ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu*" [Mat 5:48]. Kuwa mtakatifu ni uhuru kamili ndani ya Mungu.

- *Katika imani tunamsadiki Kristo ambaye amezaliwa na Mama Bikira Maria. Huyu Bikira Maria, Baba alimbariki Kwa Baraka zote za rohoni, katika ulimwengu WA roho, ndani yake Kristo, Na akamchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili awe mtakatifu na bila hatia mbele zake katika upendo.*
- *Katika imani binadamu anafanywa mwana wa Mungu kwa kupewa uwezo wa kuwa mfano wa Kristo. Hali hii humwezesha kutenda yaliyo mema. Katika umoja Na Mwokozi wake mwanafunzi hupata ukamilifu WA mapendo, yaani utakatifu.*

- *Njia ya ukamilifu hupitia kwa njia ya Msalaba. Hakuna utakatifu bila majikatalio na bila vita vya kiroho. Maendeleo ya kiroho ni pamoja Na kujinyima, kujitesa kunakopelekea pole pole kuishi siza za heri kwa amani na furaha.*
- *Wito wa utimilifu wa maisha ya Kikristo na wa wa ukamilifu wa upendo wanapewa wale wanaomsadiki Kristo wa kila cheo na hali ya maisha. Wote wanaitwa kuwa watakatifu. Utimilifu wa Kikristo una mpaka mmoja tu, ule wa kutokuwa na chochote.*

**Tafakari ya Maandiko Matakatifu**
*Law 11:44-45; 19:2; 20:7, 26; 21:8; 22:32; Kut 19:12; 16;23; 2 Sam 6:7; Kut 30:29; Eze 33:15; Bar 3:9; Ebr 4:12; 1 Pet 1:23; Yn 3:12; 1 Yoh 5:12. KKK* **2015, 1709, 2015,492...2013-14, 2028**

**Tuombe**
Ewe Maria, uliyejaa neema na huruma, kwa msaada wako, umewaokoa Wakristo kutoka magonjwa na matatizo mengi, nisaidie na uniweke huru dhidi ya uvivu wa sala na kutolitumikia Kanisa unaoniandama, nakuomba, walinde watu wema ili wawe wakarimu na watunze wanyonge wa jumuiya yetu, na pia uwavute watu wote wapate kufanya majuto ya kweli, ili ukweli na ufalme wa Yesu Kristo uweze kutawala ulimwengu wote, ili utukufu wa Mungu uenee na watu wote wawe watakatifu. Amina!
*Baba yetu….x3; Salamu Maria…x3; Atukuzwe Baba….x3 Salamu Malkia…..*

## SIKU YA NANE

### Dhambi
*"Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu" [Warumi 3:23]*

Dhambi ni kosa dhidi ya akili, ukweli na dhamiri sahihi. Ni kushindwa kuwa na mapendo kweli kwa Mungu na jirani kwa sababu ya mapendo potofu ya mambo fulani. Hujeruhi tabia ya mtu na kuharibu mshikamano wa kibinadamu. Dhambi ni kumwasi Mungu kwa kutaka kuwa "sawa na miungu". Hivyo basi dhambi ni kujienda mwenyewe mpaka kumdharau Mungu.

Bwana ametufundisha kuwa mzizi wa dhambi umo ndani ya moyo wa mtu, katika utashi wake huru, *"moyoni hutoka mawazo mabaya, uuaji, uzinzi, uasherati, wizi, ushuhuda wa uwongo na matukano; hayo ndio yamtiayo* mtu unajisi [Mt 15:19-20]. Moyoni pia hukaa upendo, msingi wa kazi njema na safi, ambao dhambi hujeruhi.

- ***Dhambi ya Mauti****: huaribu yoendo katika moyo wa ntu kwa uvunjaji mzito wa sheria ya Mungu, inamgeuza mtu mbali na Mungu ambaye ndiye kikomo chake kwa kupendelea kitu kidogo kuliko yeye.*
- *Dhambi ya mauti hutendwa kwa ujuzi kamili, na kutaka kwa makusudi.*
- ***Dhambi ndogo [nyepesi]:*** *Inadhoofisha mapendo, inaonyesha mapendo ya viumbe yasiyo na taratibu; inazuia maendeleo ya roho katika zoezi la fadhila na kuishi maisha mema. Dhambi ndogo haimwondolei mkosefu neema ya utakaso, urafiki wa Mungu, na furaha ya milele.*

**Ukweli kuhusu dhambi**

Mtume Paulo atueleza kuwa sote tumetenda dhambi, na kwa hiyo hali tumepungukiwa na utukufu wa Mungu [Rum 3:23]. Naye Mtume Yakobo atueleza kuwa tukisema kuwa hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu. Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondelee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote. [1 Yoh 1:8-9].

**Tafakari ya Maandiko Matakatifu**

*Mwa 3; Rum 7:14-24; Lawi 15:19; 1 Kor 15:21-22; Mt 12:32; Ebr 6:4-6; 10:26-31; Yn 8:21; 1 Yoh 5:16. Rejea Sakramenti ya upatanisho.*

**Tuombe**

**Ewe Maria, Mnara wa Kanisa na** Msaada **wa Wakristo, nakuomba unisaidie niwe na imani dhabiti na nitunze uhuru wa watoto wa Mungu. Kwa msaada wa neema, ninaapa kuwa mtii kwa baba mtakatifu na maaskofu walio katika ushirika naye, nikiwa na hamu ya kuishi na kufa katika imani ya Kanisa Katoliki, ambapo kuna matumaini ya uzima wa milele.Amina!**

*Baba yetu….x3; Salamu Maria…x3; Atukuzwe Baba….x3 Salamu Malkia…..*

## SIKU YA TISA

### Huruma ya Mungu

*"Tazama, nimekuchora katika viganja vya mikono yangu, kuta zako ziko mbele zangu daima" [Is 49:16*]

Mungu ni mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; na hapo Musa anamwungama Bwana kuwa ni Mungu anayesamehe[ Kut 34:5-6; 34:9]. Jina la Mungu, "Mimi Niko' au "Aliyeko" laonyesha uaminifu wa Mungu licha ya dhambi ya uasi wa watu na adhabu wanayostahili; anawaonea huruma watu elfu elfu. Mungu anaonyesha huruma yake:

- *Kwa kumtoa Mwanawe wa pekee. Kwa kutoa uhai wake ili kutukomboa na dhambi.*
- *Yesu anafunua kwamba hata Yeye anachukua jina la Mungu.*

- *Mungu anatujalia mahitaji yetu yote;* kwa *kutufanya wana anakotujalia.*
- *Mungu anaonyesha uweza wake mkubwa, hasa kwa kusamehe dhambi kwa hiari.*
- *Mungu alituumba bila sisi, lakini hakutaka kutuokoa bila sisi; kupokea huruma yake ni lazima kukikiri makosa yetu.*

Kupata huruma ya Mungu twadaiwa kuwasamehe wale wote wanaotukosea kwa kuungama dhambi zetu, mioyo yetu inafungukia neema yake. Toba ya kweli ni kuwaombea wote ambao wametukosea na wale ambao tumekosea huruma kwa Mungu na msamaha wa dhambi.

**Tafakari ya Maandiko Matakatifu**

*Hosea 1:66; 2;1,23; Yer 31:20; Isa 49:14-16; 1 Yoh 4:10,19; Rum 11:29; Zab 100:5; 136; 1 Yoh 3:1-2; Kumb 7:37; 7:8:10:15*
*KKK* **210-11,270, 2100, 1847, 2840,**

**Tuombe**

**Mama mkarimu Sana, katika kila kizazi, unapenda kiwe Wakristu, nisaidie na msaada wako katika maisha, hasa wakati wa kifo changu, ili baada ya kukupenda na kukuheshimu hapa ulimwenguni, nipate kuja kwako huko mbingu milele. Amina!**

*Baba yetu….x3; Salamu Maria…x3; Atukuzwe Baba….x3 Salamu Malkia…..*

## UTARATIBU WA KUENDESHA IBADA YA NOVENA KWA BIKIRA MARIA MSAADA WA WAKRISTO

Wakristo ambao wanapenda kupata baraka na neema katika maisha yao ya Ukristo wapaswa kuwa na ushirika wa ndani na Bikira Maria. Unataka kuwa mtakatifu? Jenga ushirika wa ndani na Bikira Maria kwa kusali rozari, kusoma mapokeo ya Kanisa ili umjue Mama wa Mkombozi. Namna ya kusali pamoja na Bikira Maria; ufuatao ni utaratibu wa ibada ya Bikira Maria.

### 1. Utangulizi

*Wimbo wa Bikira maria*
*Ishara ya Msalaba… na kama kawaida ya ibada.*

### 2. Sala

***Sala ya Mwanzo***

**Tuombe**

Ewe Mungu Mwenyezi wa Milele, tunakushukuru kwa upendo wako unaotujalia kwa njia ya Mwanao Yesu Kristo. Neno alikaa kwetu na akatwaa mwili kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Ulimpenda Bikira Maria awe Mama wa Mwokozi na wa wanadamu wote. Tunakuomba utujalie neema na ulinzi wako siku zote. Na kwa msaada wa maombezi yake tupate ahadi za uzima wa milele. Tunaomba hayo kwa njia ya Kristu Bwana wetu. Amina!

### 3. Mafundisho

*Waamini wote hukaa na kusikiliza mafundisho ya Bikira Maria katika kitabu hiki, au Mt. Yohane Bosko na pia mafundisho kuhusu Maandiko Matakatifu kadiri imepeanwa kwa siku.Pia sehemu za injili zifuatazo zaweza kutumika.*

Luka 1:26-38; Luka 1:48; Luka:36-39; Luka 2:21, 22, 40; Luka 1:46-49;Luka 2:22-24; Luka 1:48, 2:24; Matendo 1:12-14;Yohana 19:25-27

Baada ya fundisho kumhusu Bikira Maria na kusoma sehemu ya Injili, wanachama wanaweza kugawanyika katika makundi na

kutafakari juu ya Bikira Maria kadiri walivyofundishwa. Sala ya siku na tafakari yake inasomwa.

**Sala za waamini**

Hatua inayofuata ni sala za waamini, halafu zinafuata zile

**5. Sala ya Rozari**

*Sala ya Rozari ya Bikira Maria pamoja na Litania yake*

**6. Sala ya Mwisho**

**Sala ya Mwisho**

Bikira Maria Msaada wa Wakristo, wewe uliye mtakatifu sana tunakukimbilia tukiomba msaada wako. Wewe ni Mama ambaye hauwezi kumsahau Mwanao. Tunakuomba utujalie msaada wa daima katika maombi yetu, na hasa katika mahangaiko na taabu na katika majaribu ya kila siku. Uwape msaada wako wa kimama wale wote wanaoteseka. Wasaidie maskini na wadhaifu, waponye wagonjwa, waongoe wadhambi. Tunajiweka katika ulinzi wako pamoja na familia zetu. Utujalie imani dhabiti na miito mingi ndani ya Kanisa. Tunakuomba Ewe Maria Msaada wa Wakristo, utujalie moyo wa kukupenda nyakati zote na utuelekeze mbinguni kwa Mwanao. Amina!

**7. Litania ya Bikira Maria**

**LITANIA YA BIKIRA MARIA**

Bwana utuhurumie
Bwana utuhurumie
Kristu utuhurumie
Kristu utuhurumie
Bwana utusikie
Kristu utusikilize

Baba wa mbinguni, Mungu **utuhurumie**

Mwana, Mkombozi wa dunia, Mungu **Utuhurumie**
Roho Mtakatifu, Mungu, Utuhurumie
Utatu Mtakatifu m Mungu Mmoja **,** **utuhurumie.**
Maria Mtakatifu….Utuombee
Mzazi Mtaktifu wa Mungu,
Bikira Mtakatifu, mkuu wa mabikira….
Mama wa Kristu,
Mama wa neema ya Mungu,
Mama Mtakatifu sana,
Mama mwenye usafi wa moyo,
Mama usiye na doa,
Mama usiye na dhambi,
Mama mpendelevu,
Mama Msaajabivu,
Mama wa shauri jema,
Mama wa Mwumba,
Bikira Mwenye utaratibu,
Bikira mwenye heshima,
Bikira mwenye sifa,
Bikira mwenye enzi,
Bikira mwenye huruma,
Bikira amini,
Kioo cha haki,
Kikao cha hekima,
Sababu ya furaha yetu,
Chombo cha neema,
Chombo cha hekima,
Chombo bora cha ibaada,
Waridi lenye fumbo, Mnara wa Daudi,
Mnara wa pembe,
Nyumba ya dhahabu,
Sanduku la Agano,
Mlango wa mbingu,
Nyota ya asubuhu,
Afya ya wagonjwa,

Makimbilio ya wakosefu,
Mfariji wa wenye uchungu,
Msaada wa Wakristo,
Malkia wa Malaika,
Malkia wa Mababu,
Malkia wa Manabii,
Malkia wa Mitume,
Malkia wa Mashahidi,
Malkia wa Waungama,
Malkia wa Mabikira,
Malkia wa Watakatifu wote,
Malkia uliyeumbwa pasipo dhambi ya asili,
Malkia uliyepalizwa mbinguni,
Malkia wa Rozari Takatifu,
Malkia wa Amani.

Mwana kondoo wa Mungu, uondoaye dhambi za dunia, utuhurumie x3

**K:** *Utuombee, Mzazi Mtakatifu wa Mungu.*
**W.** *Tujaliwe ahadi za Kristu.*

**Tuombe**
Ee Bwana, twakuomba utujalie sisi watumishi wako tuwe siku zote na afya ya roho na mwili; na kwa maombezi matukufu ya Maria Mtakatifu, Bikira daima, tuopolewe na mashaka ya sasa, tupate na furaha za milele. Kwa njia ya Kristu Bwana wetu. Amina!

**Kumbuka**
**Kumbuka, ee Bikira Maria mwenye rehema, haijasikika kamwe kwamba ulimwacha mtu aliyekimbilia ulinzi wako, akiomba shime kwako, akitaka umwombee. Nami kwa matumaini hayo, nakukimbilia, ee Mama, mkuu wa mabikira; nakuja kwako, nasimama mbele yako nikilalamika**

**mimi mkosefu, ewe Mama wa Neno wa Mungu, usiyakatae maombi yangu, bali uyasikilize kwa wema, na unitimizie. Amina!**

## 8. Wimbo wa Bikira Maria

## MISA YA MTAKATIFU YOHANE BOSKO

**Tarehe 31 Januari**

Antifona: Njoni, enyi wana, mnisikilize, nami nitawafundisha kumcha Bwana, mtukuzeni Bwana pamoja nami, na tuliadhimishe jina lake pamoja [Zab 34:11, 31]

**Sala ya Mwanzo**

Ee Bwana Mungu wetu, katika maongozi yako ya ajabu umetujalia Mtakatifu Yohani Bosko awe baba na mwalimu wa vijana. Huyo mtumishi wako mwaminifu, akiongozwa na Bikira Maria alijituma katika utume wa vijana kwa ajili ya manufaa ya Kanisa. Utujalie moyo ule ule wa kutafuta roho za watu, hivi kukutumikia Wewe uliye peke yako Mwema. Tunaomba hayo, kwa njia ya Kristo Bwana wetu, anayeishi na kutawala nawe katika umoja wa Roho Mtakatifu, Mungu daima na Milele. Amina

**Kuombea Dhabihu**

Ee Bwana pokea dhabihu zetu tunazokutoa kwa uchaji. Tunakuomba utujalie ibada hii itusaidie tukupende kuliko vyote, na maisha yetu yageuke kuwa wimbo wa utukufu wako. Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu. Amina!

***Prefasio***

**P. Bwana Awe nanyi**

*W. Awe Pia nawe*

**P. Inueni Mioyo**

*W. Tumeinua kwa Kwa Bwana*

**P. Tumshukuru Bwana Mungu wetu.**

*W. Ni vema na haki*

Kweli ni vema na haki tukushukuru daima na po pote, ee Bwana, Baba mwema, Mungu Mwenyezi wa milele,

kwa njia ya Kristo Bwana wetu.
Baba mwenye upendo wa milele, umemteua Mtakatifu Yohani Bosko katika Kanisa lako awe baba na rafiki wa vijana ili kuwaongoza katika njia ya uzima.
Ulimpa maono ya kinabiii ili kuwaandaa vijana kukabili maisha kwa matumaini, uaminifu na imani iliyo hai. Akiangazwa na Roho Mtakatifu, aliunda familia kubwa ili kuendeleza utume wake po pote duniani kama baba na mwalimu wa vijana.
Kwa hiyo, sisi tuliokusanyika katika adhimisho hili, pamoja na majeshi ya malaika na watakatifu wote twaimba wimbo wa utukufu wako tukisema kwa furaha:
*Mtakatifu, Mtakatifu…………………………….*

**Sala Baada ya Komunyo**
Ee Baba, umetulisha kwa Sakramenti ya wokovu, tunakuomba utusaidie kuiga mfano wa Mtakatifu Yohane Bosko kuwaelekeza watu kwa Kristo aliye chemichemi ya uzima na utakatifu. Tunaomba hayo kwa Njia ya Kristo Bwana wetu. Amina.

**Baraka Kuu**

Bwana aliye chanzo cha kila nia njema awalinde daima kwa neema yake na kudumisha uaminifu wa ahadi zenu za Ubatizo. Amina
Kristo aliye Mchungaji Mwema awawezeshe kuwatumikia jirani zenu kwa uchangamfu na upendo wa Mtakatifu Yohani Bosko. Amina

Bwana awajalie ninyi nyote mlioadhimisha Sikukuu hii kwa furaha ya kutembea katika imani, matumaini na mapendo. Amina.
***Na Baraka yake Mungu Mwenyezi + ya Baba, na ya Mwana, Na ya Roho Mtakatifu, iwashukie na kukaa nanyi daima nanyi. Amina!***
Nendeni na Amani
**W. Tumshukuru Mungu**

## SALA YA MISA

### SIKUKUU YA MARIA MSAADA WA WAKRISTO 24 Mei

**Sala ya Mwanzo**

Ee Bwana Mungu, ulimchagua Bikira Maria awe Mama na Msaada wa Wakristo, kwa msaada wa sala zake, lijalie Kanisa nguvu ya Roho Mtakatifu, ili katika uvumilivu na upendo waamini washinde majaribu yote na kushiriki ushindi wa Kristo Mwanao. Anayeishi na kutawala, katika umoja wa Roho Mtaktifu, Mungu, daima na milele. Amina

**Sala kwa ajili ya Vipaji**

Baba, Tunakuomba upokee , sala na vipaji watu wako wanakutolea katika sherehe hii ya Bikira Maria Msaada wa Wakristo, kwa maombezi yake , tujalie imani, matumaini na upendo, ili tufanana na Kristo Bwana wetu , ambaye alijitolea Mwenyewe kwa ajili ya uhai wa ulimwengu. Anayeishi na kutawala daima na Milele. Amina.

**Preface**

**P. Bwana Awe nanyi**

*W. Awe Pia nawe*

**P. Inueni Mioyo**

*W. Tumeinua kwa Kwa Bwana*

**P. Tumshukuru Bwana Mungu wetu.**

*W. Ni vema na haki*

Kweli ni vema na haki tukushukuru daima na po pote, ee Bwana, mwema , Mungu Mwenyezi wa milele kwa njia ya Kristo Bwana wetu. Nasi katika Sikukuu hii ya Bikira Maria Msaada wa Wakristo, tukutukuze kwa shangwe ipasayo. Yeye, mtumishi wako mnyeyekevu na mfano wa fadhili zote, alishiriki mpango wako wa upendo, katika utii wa imani na mapenzi katika utume wa Kristo Bwana wetu. Kushirikiana naye katika Utukufu, anaendelea utume wa Kanisa: Kwa moyo wa kimama anawasaidia wanawe katika mahangaiko na hatari, katika safari ya kuelekea Mbingu ya Yerusalemu. Kwa zawadi ya wema wako,

mbingu na dunia huunganika katika shangwe kwa kuimba wimbo mpya.

**Sala Baada ya Kumunio**
Baba, umetulisha na mkate wa mbinguni, Yesu Kristo, aliyezaliwa na Bikira Maria na akafufuka kama tunda la kwanza la kizazi kipya; tujalie tufanywe upya na tushiriki katika Ufalme wako. Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu.

**BARAKA KUU**
Mungu amependa, Maria awe msaada wa Wakristo, awashushie baraka zake.

**W. Amina**
Naye Yesu Kristo, ambaye alishinda mauti msalabani na kutupatia Maria kuwa Mama yetu, awajalie mshiriki uzima wa milele.

**W. Amina**
Roho Mtakatifu aliyewashukia Mitume waliokuwa pamoja na Bikira Maria, awafanye muwe mashahidi wa ufufuko duniani.
**W. Amina.**

*Na Baraka yake Mungu Mwenyezi, ya Baba na Mwana, + na Roho Mtakatifu iwashukie na kukaa nanyi daima. Amina!*

Nendeni na Amani
**W. Tumshukuru Mungu**

## KALENDA YA WATAKATIFU NA WENYEHERI KATIKA SHIRIKA LA WASELISIANI WA DON BOSKO

**JANUARI**

15. Januari: Mwenyeheri Louis Variara, - Padre – (Kumbukumbu)

22. Januari: Mwenyeheri Laura Vicuńa, kijana (Kumbukumbu ya hiari)

**24. Januari: Mtatkatifu Fransisko wa Sale – Msimamizi wa Shirika la Waselisiani (Sikukuu**)

30. Januari: Mwenyeheri Bronislas Markiewicz, Padre (Kumbukumbu ya Hiari)

**31. Januari: Mtakatifu Yohane Bosko, Padre –Mwanzilishi wa Shirika la Waselesiani wa Don Bosco na Mabinti wa Maria Msaada wa Wakristo na pia Ushirika wa Maria Msaada wa Wakristo (Sherehe**)

**FEBRUARI**

**1. Februari: Kumbukumbu ya Wazazi wa Waselesiani (Misa husomwa katika vituo vyote vya Waselesiani wa Don Bosko)**

7. Februari: Mwenyeheri Pius IX, Papa (kumbukumbu ya hiari)

9Februari: Mwenyeheri Eusebia Palomino Yenes, Bikira (Kumbukumbu kwa Mabinti wa Maria Msaada wa Wakristo)

**25 Februari: Wat. Mashahidi Louis Versiglia, Askofu na Callistus Caravario, Padri (Sikukuu)**

**MACHI**

**19 Machi Sikukuu ya Mtakatifu Yosefu mlinzi na msimamizi ya Shirika la Waselesiani.**

**MEI**

**6 Mei: Mt. Dominiko Savio, kijana (Sikukuu)**

**13 Mei: Mt. Maria Domeniko Mazarello, Bikira (Sherehe kwa mabinti wa Maria Msaada wa Wakristo**)

16 Mei: Mt. Louis Orione, Padre (Kumbukumbu ya hiari)

18 Mei: Mt. Leonard Murialdo, Padre (Kumbukumbu ya hiari)

**24 Mei: Sherehe ya Maria Msaada wa Wakristo- Bikira Maria ndiye Msimamizi Mkuu wa Shirika la Waselesiani wa Don Bosco na Mabinti wa Maria Msaada wa Wakristo (Sherehe)**

29 Mei: Mwenyeheri Joseph Kowalski, Padre na Shahidi (Kumbukumbu)

**JUNI**

12 Juni: Mwenyeheri Francis Kesy na wenzake, mashahidi (Kumbukumbu ya hiari)

23 Juni: Mtakatifu Yosefu Cafasso, Padre (Kumbukumbu).

**JULAI**

7 Julai: Mwenyeheru Maria Romero Meneses, Bikira (Kumbukumbu ya Hiari)

**AGOSTI**

2 Agosti: Mwenyeheri Augustus Czartoryski, Padre (Kumbukumbu ya Hiari).

26 Agosti: Zephrinus Namuncura, kijana (Kumbukumbu ya Hiari).

**SEPTEMBA**

22 Septemba: Wenyeheri Joseph Calasanz Marques na Henry Saiz Aparicio, Padre na wenzake, mashahidi (Kumbukumbu).

**OKTOBA**

5 Oktoba: Mwenyeheri Albert Marvelli (kumbukumbu ya hiari).

13 Oktoba: Mwenyeheri Alexandrina Maria da Costa, Bikira (kumbukumbu).

24 Oktoba: Mt. Louis Gaunella, Padre (Kumbukumbu ya hiari).

**29 Oktoba: Mwenyeheri Mikaeli Rua, Padre (kumbukumbu**).

**NOVEMBA**

13 Novemba: Mwenyeheri Artemides Zatti, Mtawa (Kumbukumbu ya Hiari).
15 Novemba: Mwenyeheri Madeleine Morano, Bikira (kumbukumbu ya Hiari).

**DESEMBA**

**5 Desemba: Mwenyeheri Filipo Rinaldi, Padre na mwanzilishi wa *Volunteers of Don* Bosco (Kumbukumbu).**

**Kumbukumbu ya Waselesiani Marehemu**

*Tumshukuru Mungu kwa Waselesiani walioleta karama ya Mtakatifu Yohane Bosko hapa Afrika Mashariki. Wengi wa hao Waselesiani ndio walianzisha vituo vingi vya Don Bosko ambavyo vinawafaidi vijana na watoto katika Afrika Mashariki. Walijitolea kwa hali zote. Nyakati walifika walipata shida nyingi sana, hasa lugha ilibidi wajifunze lugha zetu na tamaduni zetu ili tupate kukombolewa. Wengi wao ndio waliweka misingi ya vituo vyote vya Don Bosko tulivyo navyo. Hivyo basi tuwaombea kwa Mungu siku zote. Ni wao walileta utamaduni wa Waselesiani na pia kueneza ibada kwa Maria Msaada wa Wakristo.*

| Mwezi | Jina | Mahali alipofanya utume | Tarehe aliyoaga |
|---|---|---|---|
| **Januari** | Pd. Thomas Punchekunnel,SDB | Marsabit, Upperhil, Nzaikoni, Don Bosco Boys Town, Iringa Tz | 4.01.2017 |
| | Pd. Lee Tae Seak John | Tonj Sudan | 14.01.2010 |
| | Br. Umberto Rizzetto | Don Bosco Embu | 21.01.2017 |
| | | | |
| **Februari** | Pd. Thazhoor Chacko,SDB | Dodoma Tz, Korr, Oysterbay TZ | 08.02.07 |
| | Pd. Thomas Thayil,SDB | Don Bosco Upperhill, Moshi Tz, Dodoma Tz | 23.02.2010 |
| **Machi** | Pd. Edwin Kaigarurala | Don Bosco Didia Tz, Don Bosco Mafinga seminary Tz, Makuyu Kenya | 14.03. 2011 |
| **Aprili** | Br. Palathinkal | Marsabiti Kenya, | 16.04.1994 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Cherian,SDB | Don Bosco Boys Town Kenya | |
| | Pd. Padinjaraparambil George,SDB | Marsabiti Kenya, Korr Kenya, Don Bosco Upperhill, Don Bosco Moshi, Don Bosco Didia Tz, Don Bosco Mafinga Seminary Tz, Don Bosco Boys Town | 19.04.2012 |
| **Mei** | Pd. Puthenveettil Jacob,SDB | Don Bosco Upperhill, Don Bosco Boys Town | 02.05.2008 |
| **Juni** | Pd. Listelo Benjamini,SDB | Don Bosco Embu, Don Bosco Makuyu, Don Bosco Moshi | 11.06.2000 |
| | Pd. Pullenkannapallil Manuel,SDB | Don Bosco Mafinga, Don Bosco Korr, Don Bosco Upanga | 23.06.2005 |
| | | | |
| | Pd. Daoura Charbel A., SDB | El Obeid Sudan | 23.06.2015 |
| | Pd. Lobo Joaquim,SDB | Don Bosco Iringa Tz, Don Bosco Dodoma Tz, Don Boscko Khartoum | 29.06.2015 |
| | Br. Fernandez Gabriel,SDB | Juba Sudan, Don Bosco Iringa , Don Bosco | 22.07.2008 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Julai** | | Dodoma, Don Bosco Khartoum | |
| | Br. Pinakatt Abrahama,SDB | Don Bosco Iringa, Don Bosco Dodoma, Don Bosco Boys Town, Don Bosco Moshi | 23.07.2011 |
| **Agosti** | Pd. Popowski Bernard,SDB | Don Bosco Bombo Uganda, | 27.08.1999 |
| | Pd. Cais Demetrio,SDB | Don Bosco Siakago | 31.08.1997 |
| **Septemba** | Br. John Williams,SDB | Don Bosco Iringa, Don Bosco Moshi, Don Bosco Dar es Salaam, Don Bosco Upperhill, Don Bosco Utume Kenya | 01.09.2010 |
| | Pd. Braganza Thomas,SDB | Don Bosco Mafinga Parish, Don Bosco Upanga | 08.09.1992 |
| | Pd. Gariglio Luigi,SDB | Don Bosco Makuyu, Don Bosco Embu | 09.09.2014 |
| | Pd. Abate Luigi,SDB | Don Bosco Embu, Don Bosco Makuyu | 10.09.1993 |
| | Pd. Soreng Patrick,SDB | Don Bosco Wau, Don Bosco El Obeid, Don Bosco Khartoum, Don Bosco Juba | 16.09.2013 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Pd. Masichio Luka,SDB | Don Bosco Embu, Don Bosco Makuyu | 19.09.1994 |
| **Oktoba** | Br. Morcelli Alphonso,SDB | Don Bosco Embu, Don Bosco Oysterbay, Don Bosco Moshi, Don Bosco Dododoma, Don Bosco Khartoum | 23.10.2010 |
| | | | |
| | Pd McFerran Sean,SDB | Don Bosco Boys Town | 12.11.1998 |
| | Pd. D’Souza Crispin,SDB | Don Bosco Dodoma, Don Bosco Iringa | 13.11.2010 |
| **Novemba** | Pd. Anthony Lucrasio Pinto,SDB | Don Bosco Upperhill, Don Bosco Boys Town, Don Bosco Boys, Don Bosco Nzaikoni | 26.11.2005 |
| | | | |
| | Pd. Malieckal Joseph,SDB | Don Bosco Mafinga Seminary | 02.12.1996 |
| **Desemba** | Pd.Kizhakeyil Jacob,SDB | Don Bosco Maridi, Don Bosco Korr | 20.12.1994 |
| | Pd. Valayam Philip, SDB | Don Bosco Moshi, DBYES | 25.12.2005 |

**REJEA**

AUBRY J., *The renewal of our Salesiani Life*, New York 1984.
DESRAMAUT, F., Life *of Fr. Michael Rua Don Bosco's Successor*, 1837-1910), Rome 2010.
HUBERT J.T, - DONALD A., *Butler's Lives of Saints,* Westminster, Mary Land, 1990.
J.PUTHENKALAMA, - A. MAMPRA**,** *Sanctity in the Salesian Family*, Tamil Nadu 2002.
LENTI A.J, *Don Bosco: History and Spirit* Vol III, Rome 2008.
LENTI A.J, *Don Bosco: History and Spirit* Vol IV, Rome 2008.
LENTI A.J, *Don Bosco: History and Spirit* Vol VI, Rome 2009
LENTI A.J, *Don Bosco: History and Spirit* Vol VII, Rome 2010.

*Salesians of Don Bosco Province od Eastern Africa, Province Directory 2017-2018.*
*In dialogue with the Lord; Manual of prayer for the Salesian Communities*, New Delhi India, 2004
*Salesian Proper Offices Calendar and Liturgical Texts*, Rome 2011.
*General Chapter XXVI, "Da Mihi Animas Cetera Tolle "Salesians of Don Bosco, Rome 23 Febraury 2008.*
*THE NEW ADMA REGULATIONS, Association of Mary Help of Christians [ADMA] , Pisana Roma July 2003*

*Katekisimu ya Kanisa Katoliki*, Nairobi 2000.
*Maisha ya Watakatifu*, Tabora Tanzania 1996.
*Misale ya Waumini*, Tabora Tanzania, 1978.
*Biblia Takatifu*, Iringa 2004.
Hati za Mtaguso Mkuu wa Vatikano II, Iringa 2001.